# Protestanti



**CENTRE DE LA MISSION ORTODOKSE**
**KOLWEZI KONGO**
**2000**

# MATANGULIZI

Wandugu wapenzi katika Kristu,

Tunaishi katika wakati moja ya kusikia mafundisho ya uwongo ya makanisa mbalimbali mule munapatikana zambi nyingi kwa kuwatenganisha watu. Watu wote wanafwata Kanisa ya Mungu, lakini haina yote Kanisa munapatikana Mungu, Bwana Yesu Kristu aliaacha Kanisa moja tu duniani.

Lakini watu hawajue Kanisa gani ilio kweli wanapenda kuchunga na kufwata mafundisho na akili yao na wanakataa kufwata mafundisho ya kanisa yake Bwana Yesu Kristu, hii Kanisa ni moja, Takatifu, Katholiki (wa dunia mzima na imani ukweli), Apostoliki (wa Mitume).

Tunapenda kusaidia wandungu wetu katika Kristu, na wandugu wa Communaute Protestante kwa kujua vema mafundisho ya Bwana Yesu Kristu. Hakuna chuki katika mioyo yetu mbele ya wa ndugu wa Protestants, lakini kwa mapendo ya Mwenyezi Mungu tunaandika hii kitabu juu ya ninyi wandugu mupate kurudi katika Ekklezia Orthodokse. Tunapenda kupokea wandugu wote wenye kupenda kuzungumuza na sisi katika mambo yote ya Theologia ya Eklezia yetu.

Eklezia Orthodokse ni Mama ya ma kanisa yote, kwa sababu inachunga imani na matoleo, bila kupunguza, wala kuongeza fundisho aliacha wakati alipanda mbinguni. Matunda ya Roho ni miujiza ya Watakatifu wetu, kwani miili yao inabaki bila kuoza na inatoa arufu nzuri na manukato.

Matunda munene kabisa ni ya mtu mwenye zambi nyingi kama anafwata na kuamini Kanisa yetu ni namna ya yeye kuwa Mtakatifu, katika matendo yake vizuri.

Na ninyi wa somaji munaosoma hii kitabu inafai muwapatie watu wengine nao wasome zaidi inapashwa kuomba kwa kuwaangazia akili yao ili wafwate kanisa Orthodokse katika Mafumbo (Mysteres) yake.

Tunatumaini na baraka ya padri mkubwa wetu, padri arhim. Meletios Grigoriatis ya kama hii kitabu itasomwa kwa wa Kristiani Orthodokse, na kwa wandugu wengine kwa kupata njia ya kweli na uzima wa milele.

Kwa matakio na mapendo katika Bwana Yesu Kristu

Mission Orthodokse
Kolwezi Kongo
29-4-1991

# FUNDISHO JUU YA MAKOSA YA WA PROTESNTANTS

Hii miaka ya sasa watu wanasikia fundisho nyingi ya wa Protestants, hii wakati wa mwisho watu wanatafuta kusikia fundisho gani iko ya kweli. Mbele ya kwandika fundisho ya ki Protestants; ni lazima kwandika uzima wa mkubwa yao.

Martin Luther mwanzo wake ilikuwa mu kanisa ya Katholika. Akatoka mu mwaka 1535 na kwenda kufanya kanisa na fundisho ya uwongo.

Na uzima ya huyu mkubwa uko hivi:

Alizaliwa mu mwaka 1483 mu inchi Germania, muji Aislemben na akafunza masomo Firongili kisha akafwata mafundisho ya utawa, lakini aikupendeze. Na hakwanze kusikilizana na wazazi wake; walimupiga kila wakati na kumutosha vidonda na damu juu ya mwili wake; njoo ile ilimupatia sikitiko nyingi na akaenda kufwata masomo ya utawa, na alikuwa na umri wa miaka 22 na alikuwa na woga mingi juuya wazazi wake kwa sababu aliona gehena. Hakukuwe na kitumaini juu ya Mwenyezi Mungu ndani ya roho yake; yeye alizania ya kama Mungu ni mwenye makali, hana wa mapendo.

Mu mwaka 1507 akapadirishwa na mbele ya kufanya misa yake ya kwanza alianza kutetemeka sana mbele ya Meza Takatifu. Kwa sababu alizania ya kama Mungu ni mkali ku macho ya watu. Naye hakukuwe na utulivu ndani ya roho yake, akaona sawa Mungu ni adui wa watu. Na kisha anaongeza na kusema wale watu wanatenda zambi ni kusema Mungu asiwapende na Mungu asiweze kuwahukumu.

Wakati Jean-Calvin alikuwa mwalimu wa masomo mkubwa; ni kusema ku universiti ya muji wa Vitembergi, alifundisha mambo iliyo ya haki na alikamata barua ya Mtume Paulo (WaRoma 1,16-17); mule ndani anasema; Evangelio ya Mungu iko nguvu na inatendeka kwa watu wale wanaitumikia na kuwapa wokovu (Wa Roma 1,17).

«Mtu mwenye haki ni yule anesha kuamini: Ni kusema wokovu wa mtu unatokea kwa imani; Mkubwa wao anasema paka kwa imani njoo mtu ataokolewa si kwa saidio na kwa kazi yake, na anaongeza tena; mtu asiweze kufichua zambi zake ata kidogo ku macho ya Mungu. Na kisha anasema Mungu asiweze kuweka mtu ndani ya moto na kisha akageuza na kusema; Mungu Mwenyezi hawezi kuleta malipizi kwa sababu Baba Mungu ni paka wa mapendo na Mwema kwa watu wake.

Na akiongeza akisema; mtu akianguka na zambi zake hakuna namna ya kuweza kulamuka paka Mungu njo eko na uwezo.

N.B. Tunaona ya kama mafundisho yake haina ya kweli; kwani wakati ingine anasema kweli na saa ingine anasema uwongo; yeye anasadiki Biblia asema ni pumuzi ya Mungu na saa ingine hasadiki, kwa sababu Mtume Yakobo (2,20) anasema: «Imani pasipo matendo ni ya bure: Nikusema haiko na faida kwa Mungu, na kisha Jean Calvin akasema maandiko ya Mtume Yakobo ni ya sipo faida kwake. Njoo kwa hii mambo anakatala na mafundisho ya Yoane maneno ya Ufufuo.

# KANISA YA ROMEO-KATHOLIQUE

Kutoka kwa Yoano Calvin mu Catholika iko hivi: Kila wakati yeye anasema kosa ya pape wa Roma; ni ya kukatala Bwana Yesu Kristu. Asema Pape hana mtu wa kweli, apa tunaona ni mtu wa wongo, yeye akasema fasi ya Monasteri ni ya zambi, kwa maonyo yake mkubwa Calvino; hii fasi anakatala kazi ya utawa akiongeza asema wa padri Catholika kama wanafanya misa ya mtu mgonjwa wanaomba feza mingi na wanafundisha asema wingi wa feza ni wingi wa utulivu wa roho yako. Na Baba Calvino alisikia sikitiko mingi kwa hivi pape alianza kuomba feza kwa watu juu ya kuwasamehe zambi zao.

Martin Luther anatushi Pape kwa matushi mingi, na yeye anazarau Kanisa ya pape inatokea kwa shetani apana kwa Mwenyezi Mungu na Kanisa yake ni uwongo na kisha tena ni ya shetani na; anaharibisha ma roho za watu. Pape ni mfalme wa watu wabaya na kisha ni mutumishi wa shetani na jina lake ni nguruwe wa shetani na hii matushi wanamutushi kwanza mwanzo wa uzima wake na mwisho. Karibu na mwisho wa uzima wake aliandika kitabu kwa mkono; na anasema katika maisha yangu yote nilikuwa mgonjwa juu yako; na kwa lufu yangu itakuwa yako wewe pape.

N.B. Hii ubaya yote anaona mbele ya Pape njoo mpaka wa mwisho wake. Yeye alikwenda kwa kuwa mutawa, lakini kuingia kwa kazi ile; haikukuwe kwa mapendo yake yeye mwenyewe. Ni kusema ndani ya roho yake hakukuwe na furaha juu ya ile kazi, na alitafuta kutosha nguo ya Umoine na kufanya mahubiri mbaya juu ya wale watawa, na waminifu wengi walimufwata sababu ya mafundisho yake, kwani walipenda kuacha uzima wa utawa na kufanya ndoa.

Mu mwaka 1524 akatosha watawa wake na kuwapeleka mu mji na akakamata fungulo ya ku Monasteri kuleta kwa mkubwa wa ile muji; na yeye akatosha nguo zake ya utawa na kuvaa sawa watu wote. Na kisha akahubiri mambo ya ndoa kwa watu wote. Hii kazi yake ilileta kelele nyingi kwa watu. Akaanza kusumbulia na watu masemo mbaya.

Walimuonyesha juu ya kurudi ku Monasteri yeye akakatala na kufanya ndoa.

Kweli, pale alifika na umri wa miaka 42 akafanya ndoa na Dada moja jina lake Katerine Bora alikuwa na miaka 27 na tarehe ya ndoa yake ilikuwa mu 11-6-1525. Kama unafanya zambi, unasaidia Yesu Kristu, utakuwa karibu na Bwana Yesu, na yeye bila kutubu, Mungu hatawahurumia watu wote. Kama mtu moja hafanye zambi ule mtu eko na majovuno njoo mafundisho ya Bwana Martin Luther.

Mtumishi wake moja mzuri akasema iko lazima kutimiza mafundisho ya Biblia kwa sababu mtu hasiweze kufanya yote ao kuyatimiza. Katika ndoa ya Martin Luther alisikia furaha kidogo, na sikitiko ndani ya roho yake na hii sikitiko yake ilikuwa juu aliacha kazi ya Umoine. Na yeye aliona misterio ya ndoa ni ya bure kwake. Anasema kama munaachana na bibi yako, kuko namna ya kubeba mutumishi wako kuwa mwanamuke? Ni kosa kwa sababu yeye eko nakatala sala ya ndoa. Anafundisha asema mtu hana mkubwa wa zambi yake ao uhuru juu ya mwili wake na kwa mapenzi yake, mtu eko na uwezo wa kufanya zambi na mtu mwingine?

Alisikia nzuni ya kuacha nia yake, kwa maana aliacha uzima wa utawa; akisema: Mtu eko na nia, lakini hana uhuru juu yake. Mungu yeye mwenyewe eko na uwezo. hii mawazo yake ndiyo kosa mkubwa. Kwa sababu kila mtu atahukumiwa kwa maana ya matendo yake. Mafundisho kuleta haina juu ya maandiko Matakatifu; yeye anaona Mungu sawa mwenye kuleta mateso kwa watu: Akatupa watu wengine mu gehena bila kufahamu usimamizi wa matendo yao mbaya. Na wengine kuwaingiza mu Paradizo bila kufanya ao kuisha vema matendo yao. Watu wa kundi lake wanasadiki hii mambo! «Kama Mungu anaandika wokovu wangu, nitaokolewa, kama asiaandike, nitaenda mu gehena, bila kusaidia nafsi yangu». Saa yote anapata woga wa upumbafu, akisadiki ya kama shetani anamufwata kwa mwenendo wa miguu yake.

Anawaonyesha watu majivuno yake, akisadiki ya kuwa yeye peke yake anauwezo wa kutambua vizuri maneno ya Biblia. Kwa wengine wanasema weko na roho ya ngiza, hawawezi kusikia maneno ya Biblia, hawana na uwezo wa kutambua Mungu na mafundisho yake, na anatumaini yeye kuhubiri habari njema. Anasadiki ya kuwa wa padri watakatifu hawana na Roho Mtakaitfu: Mfano Yoano Krisostomo, anaandika tena ya kama desturi ni kitu kisipo na faida.

Anapenda Kanisa Orthodokse, akisema huyu ni Mama wa ma Kanisa yote. Hakuna uzwizi ya mambo hata moja juu ya sisi kukataa hii Eklezia iliyo na mashaidi mengi sana.

Na mambo hii yote ya Watakatifu iliisha tangu mwaka 1400 ndani ya Kanisa Orthodokse ya Kiyunani; Martin Luther anasikia ya kama Eklezia Orthodoksi ilikuwa ya kwanza mu dunia mzima. Yeye anaita Kanisa ya Orthodoksi sawa ya mashaidi ya Watakaitfu na Mtakatifu Theologo anasema Kanisa hii inafata fundisho ya Mitume bila kosa.

Martin Luther kwa akili yake ya majivuno na zambi yake alitosha amri ya Kanisa Orthodoksi na kufanya Kanisa yake, akiongeza watu wengi kwa kuleta makelele kwa roho na fundisho yake ilikuwa juu ya: «Mwisho ya dunia».

Tokea mwanzo ya fundisho yake, watu wengi walianguka katika zambi. Anasema hivi «Sisi tuko na imani ya Bwana Yesu Kristu na hii inaenea kwa kupata wokovu wetu»; Na Martin Luther anaona hii uzima wa zambi zake anazania ya kama watu wale wanafwata njia yake. Lakini anapoteza watu wake, wakati ule alitaka kufundisha uzima wa kweli.

Na watu wake walimuonyesha wewe hautuonyesha ya kama mtu anaweza jambo mzuri na kubaki na haki mbele ya Mungu! Na wakati watu wake walimuonyesha zambi ya wengine kati yao, yeye akasema kwa fumbo ya uchungu:

«Kuishi ku siri ya usharati; na watu wa muji, wanakunywa kulewa na kufanya zambi kwa mwili zao». Na jambo hii ikamuletea Martin Luther shaka mingi ndani ya roho yake mpaka mwisho wa maisha yake. Kwa sababu uzima wake alikuwa na mifano mbaya mbele ya watu wake. Wakati aliona matengano ya watu wake; akasema hivi: Miaka itakapokuja; kutakuwa walimu wengi, fujo itapita na hata mutu moja asitaweza kutii mambo ya mwingine, na kila mtu hatatamania kujionyesha kuwa mwalimu wa kwanza.

Wakati Martin Luther aliishi, wanafunzi wake wengi walimukana na kila mmoja alijifanya kuwa mwalimu wa kweli.

Katika fumbo wanafunzi wake wanaita mwalimu wa cheo, na alikuwa mwenye uwongo, Pape mpya ni muzaifu na mwenye chuki mingi. Martin Luther akasirika kwa sababu ya mwanafunzi wake Thomas-Minsther aliandika juu ya mwalimu wake akisema: Munamupiga, munamuuwa kwa siri bila kusahau ya kama hakuna sumu mbaya ya shetani sawa mtu mwenye kuleta ugonvi. Huu mufano unafananishwa na mtu mmoja mwenye kutaka kuuwa mbwa mkali. Mambo haya yote yanaonyesha magumu ya nafsi yake. Naye Martin Luther anaona jambo yake imeshidakana. Alishikwa na woga; akiwa sawa mtu wa mazimu; akipoteza woga wa Mungu, kwa sababu ya wingi wa miaka ya uzee wake, aliteswa, akaanza kwandika kitabu mbele ya Pape na wanafunzi wake. Na aliandika tena mbele ya mwalimu wa masomo ya Iniversiti, akiwatukana na akisema: Wote ni kama nguruwe na uchafu wa gehena na makutano nyingine. Naye hakupata ukimya, hata bibi yake, hata watu wake. Rafiki yake moja, Melakton anamwandikia na kusema: Maisha ya Martin Luther ni kifungo ya mateso mingi.

Usiku wa tarehe 17-2-1546 alishikwa na ugonjwa, na ndani ya kichwa chake mulikuwa damu; na kadiri saa tatu ya usiku, bila saidio ya waganga; akafariki. Na mbele ya kufariki kwake aliuliza mwili wake akisema: Roho yangu inasikia makelele na inajiuliza asema: Wewe peke yako una haki? Na watu wote wanatenda zambi? Na kama wewe unapeleka watu wengi katika gehena? Alitetemeka moyoni mwake wakati alisikia maulizo haya. Na aligombana kwa kuonyesha ya kama nafsi yake haina na haki.

Martin Luther hakuweza kusikia faida ya ukweli ya Eklezia Orthodoksi, akifwata mafundisho na kanuni yake. Ni kwa namna hii alikuwa mkubwa wa kundi ya ukosefu, akitenganisha watu wa dunia nzima kwa sababu ya majivuno yake.

## KOSA YA PROTESTANTI

Katika hii miaka yetu ya sasa, wa Protestants wanachana katika ma kundi nyingi. Hapa mu Kongo ma kundi yao yote ni 300. Na inaendelea na kuongezaka. Hii matendo inaonyesha matenganisho ya imani, na sala ya Kanisa; Wao wanasema alama ya imani ni ya uwongo kwa maana Kanisa yao Katholika na Apostoliki hawana mumoja. Wa Protesntants hawana na matumaini ya kufwata na kupata ukweli wa Mungu, kwa sababu kila mtu anajiona sawa pape; nikusema kila mtu eko na uwezo wa kufafanua Biblia kwa namna yake. Ile anasikia; na kuweza kufanya Kanisa yake yeye mwenyewe. Mfano wa kundi ingine inayoitwa Kwaker; ilifaniwa na

mshani ya vyatu; anasema sawa Nabii na anasema anabeba mwangaza wa Roho Mtakatifu kwa Mungu.

## 1. Kukana Mapokeo Matakatifu

Kundi yote ya wa Protestants wanasema kwao, inapashwa tu paka Biblia kwa kupata wokovu. Sisi tunasadiki ya kama watu waliandika Biblia waliangaziwa na Roho Mtakatifu. Lakini Martin Luther yeye asiamini! Kwani katika Biblia ni Chemchem ingine iliyo mapokeo. Wakati tunasema Mapokeo tunasikia: «Mafundisho ya Bwana Yesu Kristu na ingine ya Mitume, hawakwandike». (Yoano 21,25). Mafundisho yake kwa wa Mitume na ingine ku makutano ya Wapadri Watakaitfu; na uzima wao, miujiza mbalimbali na ufafanusho wa Biblia kwa wa padri Watakatifu, sala ya Liturgia Takatifu, siku Kuu ya Watakatifu, Hadizi ya Kwarezima, na namna ya kufanya misterio yote ya Kanisa.

Mambo yote ni paka kwa mapokeo, sasa inatuonyesha. Kwa mfano: Tunajua namna gani vitabu vya Agano Jipya viko 27? Na paka kwa njia ya mapokeo.

Wa Protestanti wanakatala mapokeo, sasa namna gani wanajua ya kama Agano Jipya iko na Vitabu 27? Hawana na jibu juu ya hii ulizo! Na kama sisi wa Orthodoksi tunauliza fasi gani ndanio ya Agano Jipya wanaandika Agano Jipya iko na vitrabu 27? Hakuna jibu watakuwa nayo juu ya kusema. Mapokeo inatuonyesha ya kama; wakati wa mbele siku ya mapumziko ilikuwa mposho, ni sababu ya ufufuo wa Bwana Yesu Kristu inakuwa mu Juma.

Na Biblia aituonyesha hii mafundisho ni paka kwa mapokeo tunaitambua kwa kuitumainia. Kwa Mapokeo tunapata historia (Hadizi) ya Mitume wengine wa Bwana Yesu Kristu. Kwa sababu Agano Jipya inatoa paka uzima gumu, na mafundisho ya Mitume mbili nikusema Petro na Paulo. Sasa namna gani tunafahamu uzima wa Mitume wengine? Ni paka kwa Mapokeo. Bila Mapokeo atukuweze kupata namna ya kufahamu Agano Jipya. Mapokeo haina mafundisho ya watu wa bure, inatoka kwa Watawa na wa padri Watakatifu ya Kanisa Orthodokse.

Sasa tutaandika na sura ya Agano Jipya: (2 Thes. 2,15) «Basi, ndugu, simameni kwa nguvu, mushike mafundisho muliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa barua yetu». (1 Korinto 11,2) : «Ninawasifu ninyi kwa sababu munanikumbuka mimi katika maneno yote, na munashika mafundisho kama nilivyowaletea ninyi». (Filipo 4,9):«Fanyeni maneno muliyojifundisha na kuyapokea na kuyasikia na kuyaona ndani yangu, na Mungu wa salama atakuwa pamoja nanyi».

## 2.Wokovu wa watu

Sisi wa Kristu wa Orthodoksi tunasadiki Mungu, kwa anguko ya Adamu na Eva. Akili yao ilikuwa ya ngiza, mapenzi, na uharibifu iliwashika ndani yao na matakio mbaya. Lakini ndani ya nafsi zao mulibaki zawadi kidogo ya Mungu. Alipata uhuru tele; akikokotwa kwa nia ya wokovu, tena kwa njia ya uharibifu. (Wa Roma 7,14-25), Mutume Paulo anasema hivi: «Mtu anapenda kufanya kazi muzuri na asiweze kufukuza kazi mubaya, kwa sababu nguvu ya Mungu; iko ndani ya nafsi ya mtu inaleta mupango wa moyo, na hii mupango ya Mungu; mtu anapenda kufanya kazi fulani».

Hii jambo inaonyesha ya kama mtu asikufe kwa moyo; ni kusema moyo inaharibika. Kila mtu eko na sura ya Mungu ao mfano wa Mwenyezi Mungu, na hii mufano aikufwe; lakini inaharibika. Na mapendo ya wokovu inatoka kwa usulubio wa Bwana Yesu Kristu. Na ni hii neema ya Mungu inaangaza mtu na kumusaidia sababu ya yeye kuingia mu njia ya wokovu. Wokovu ina na mifano mbili:

A. Huruma wa Bwana Yesu Kristu juu ya zambi ya mtu;

B. Kupanda kwa fazila kwa kupokea neema ya utakaso;

Hiyo ni taji iko na kil;a mu Kristu juu ya kujikaza katika imani juu ya kufanya kazi iliyopendeza Mungu. Kwa sababu imanbi pasipo matendo ni ya bure, ni lufu (Yakobo 2,14). Wokovu wa Mungu kufwatana na mafundisho ya Biblia ina na mifano mbili:

Kwa nguvu, ni kusema kwa neema ya Mungu, na ya pili kwa mapenzi ya mtu. Kazi ya imani ni mafundisho ya Bwana Yesu Kristu kwa misterio ya Kanisa; mbele ya shauri ya Padri wa Roho zetu, ingine tena ni unyenyekevu mapendo kwa Mwenyezi Mungu na kwa jirani, kutubu zambi zetu, sala za Mungu. Sisi atuwezi kusadiki kupata wokovu kwa kazi zetu! Ya kwanza wokovu ni zawadi ya Mungu, na juu ya hii baraka mtu anapashwa tena kujikaza kwa kupata wokovu. Yote ni mafundisho ya Kanisa Orthodoksi.

Mafundisho ya wa Protestanti ni ingine, kwao wanasadiki ya kama, kisha kuanguka kwa mababu zetu wa kwanza Adamu na Eva, mtu alipoteza zawadi ya Mungu, na anaishi pasipo woga, mapendo na matumaini ya Mungu. Wanaandika ya kama; mtu ni mbaya kupita jiwe. Na wanasema, mtu aliisha nguvu na akili yake; na asina hata makaa ya moto kwa nguvu ya roho yake. Lakini, kama tutapokea hii mafundisho ao mfano wa wokovu ni pasipo faida kwa sababu alipoteza mfano wa uso wa Mungu, na uhuru wa akili zake. Na kama tunapokea hii mafundisho, mtu asitakuwa na namna ya kupata zawadi ya Roho Mtakatifu.

## 3. Kwa imani tunaokolewa

Martin Luther na Jean Calvin na wa kubwa wengine wa Protestanti, wanakana matendo ya imani, wakionyesha paka neema ya kimungu inaokoa watu. Kama mtu, fulani atasidiki kuriti Paradizo ataingia.

Wa Protestanti wanasema; wokovu inatoka mbinguni, na si lazima itoke kwa vitu ao kwa watu wa dunia. Hata sala moja, ao misterio inaleta neema ya Roho Mtakatifu kwa watu. Waminifu wote wanaweza kwa nafsi zao kuzungumuza na Mungu; na kubeba neema yake. Juu ya nini tunapashwa kuwa na misterio na sala ya Kanisa?

## 4.Kanisa ya Misterio

Wao wanasema Kanisa iko paka mbinguni, hakuna Kanisa duniani. Kama tutapokea hii mafundisho inatupashwa kufukuza waminifu, wa padri na misterio (Mafumbo) yote. Mafundisho ya kweli ni hii! Kanisa iko ku mbingu tena na duniani. Mfalme wa hii Kanisa eko juu mbinguni na apa duniani. Neema ya kimungu atuione; lakini wote wanapatikana mbinguni. Hii Kanisa ya dunia inawaminifu wenye kujitayarisha kwa misterio yao. Kanisa letu ni ya historia (Hadizi) ya cheo. Askofu, na juu upadirisho wao wanasema wanapata neema ya Roho Mtakatifu. Na hivi Kanisa ni moja yenye kupatikana mbinguni na duniani. Nayo Kanisa yetu Orthodoksi ni Chemchem ya mafundisho isiyo na kosa; ni shanduku ya wokovu. Inje ya Kanisa letu akuna wokovu. Njoo maana wa Protestanti wanakataa Kanisa ya dunia, ni kusema: Wanakataa misterio zake. Wanaongeza fundisho asema misterio haina na faida katika wokovu wa mtu, nayo hailetee mtu neema hata moja ya Roho Mtakatifu kwa sababu ni alama na ni makumbusho ya kueleza sisi tuko katika kundi ya ki Kristu.

Nao wanasema, hata kama wataacha misterio, hakuna hata kitu kimoja kitapotea kwa roho zao. Wanakanyaga mafundisho ya Biblia na awaeshimu mapokeo. Ndiyo; kwa sababu wao hawana na Kanisa, maana Kanisa ni misterio na ukweli. Wao wanafanya kwa kila kundi kidogo ya dini bila uzima wa misterio, na pasipo neema ya utakaso.

Martin Luther mbele alipata ubatizo, na komonyo, na kisha anakataa ubatizo na kuitika paka Komonyo Takatifu. Hii mafundisho ni ya kosa mkubwa.

## 5.Ubatizo na Krisma (Manukato Takatifu)

Wa Protestanti wanasema, ubatizo ni alama ya inje tu! Na alama hii inaonyesha ya kama Bwana Yesu Kristu anatupokea. Na hii alama hailete neema kwa Roho Mtakatifu hata kidogo. Kwa sababu mtu fulani anabeba hii neema paka kwa imani; ubatizo aisafishe zambi ya watu wa kwanza; na hailete utakaso. Watoto hawana ndani ya Kanisa kwa sababu hawawezi kusikia. Lakini Bwana Yesu Kristu anasema, mwache watoto kidogo waje kwangu kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao. Kwa sababu wao wanakataa ubatizo sawa misterio, ndiyo maana wengi sana pamoja na watoto wao wanaishi na hali ya kipagano. Wanakataa mafundisho ya Yesu Kristu: (Matayo 28,19) «Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana, na la Roho Mtakatifu».

Na sura zingine (Marko 16,16). (Yoano 3,5). (Matayo 2,28). (Wa Roma 6,3-4). (WaGalatia 3,27). (Wa Kolosayi 2,12). (Tito 3,5). (1 Petro 3,21).

Mafundisho yetu sisi wa Orthodoksi, ubatizo ni misterio inaondosha zambi na ndiyo alama ya wanamwamini Bwana Yesu Kristu: Na wa Protestanti wanaitikia mtu kupata ubatizo hata mara mbili, kwa sababu hawasadiki ya kama ni misterio.

Juu ya Krisma, wanaikana sawa misterio tena sawa alama, na wanasema hawaone ndani ya Evangelio fasi hata moja inasema juu ya hii misterio. Lakini sisi tutaonyesha sura ya vitabu mbalimbali vilivyotuonyesha ya kama misterio ya Krisma ilichapwa kwa wa Kristu kisha pale Mitume waliwabatiza. (Matayo 8,17). «Wakaweka mikono yao juu yao, nao wakapokea Roho Mtakatifu». Na kitabu kingine (Matayo 19,6). (2 Korinto 1,21). (1 Yoano 2,2). (1 Yoano 2,27).

«Mafuta yale muliyopata kwake ya nakaa ndani yenu...». Sisi tunaona Mitume tangu zamani, wanaleta hii misterio kwa mafuta.

## 6. Komonyo  Takatifu

Wa Protestanti wanakataa Komonyo sawa Misterio, na wanasadiki ya kama ni alama tu! Ya makumbusho ya siku ya kazi ine mkubwa Karamu ya Bwana Yesu Kristu ao ya Mitume wake. Wanasema Kristu anabaki, siku zake ndani ya roho, nayo Komonyo hii kitu bure, sababu wao wanazungumuza na Bwana Yesu kwa roho, naye anakaa ndani mwao.

Ni kusema akili yao iko juu ya Agano Jipya na mafundisho ya Yesu Kristu. Ndiyo maana wanakataa Komonyo sawa misterio. Martin Luther, alikataa kwamini ya kama mukate na divai inageuka kweli na kuwa mwili na damu. Siku moja katika makutano, mmoja wao alisema juu ya hii kosa, na yeye alijibu kwa kasirani na kusema, «Apana kutafuta, apana kusungukmuza, paka imani, imani, imani». Mukate na divai tunaona; haina mwili na damu ya Yesu Kristu? Lakini inafanana tu! Ndiyo maana ni damu tu! Wakubwa wengine wa Protestanti: Mfano wa Zviglios na Calvino wanazarau misterio mkubwa; wakisema: Kusadiki mukate na divai kuwa mwili na damu ni sala ya uchafu.

Lakini mafundisho ya kweli ya Yesu Kristu ni hii: (Matayo 26,26-28). «Na wakati walipokuwa wakikula Bwana Yesu Kristu akatwa mukate akaubariki na kuuvunja, akawapa wanafunzi wake akasema: Twaeni ninyi wote huu ni mwili wangu...Kunyweni ninyi wote hii ni damu yangu...(Marko 14,22-24); (Luka 22,19-20) (Yoano 6, 53): «Basi Yesu Kristu akawaambia, kweli kweli ninawaambia ninyi, kama hamukule mwili wangu na kunywa damu yangu; hakuna uzima ndani yenu».

«Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli», «Yeye mwenye kula mwili wangu na kunywa damu yangu, anakaa ndani yangu, na mi ndani yake».

Tangu mwanzo, sisi tunachunga mafundisho ya misterio yote toka mwanzo na mpaka sasa.

## 7. Maugamo Takatifu

Wa Protestanti wanakataa Misterio ya Maugamo takatifu. Wanasema: Wakristu wanaweza kufanya kitubio yao mbele ya Mungu; na mbele ya watu. Kwa mfano watu wa wili wakikosana, wakati wanasikiliza na, hii njoo kitubio inaonekana mu miaka mia tano.

Yoano Calvino anaandika: Kanisa haijue kitubio ya kufanya zambi; ila tu ya Mungu. Ni lazima kufanya kitubio paka mbele ya Mungu kwa sababu ni yeye anahurumia. Na iko namna ya kutubu mbele ya Mungu ao mbele ya watu. Hii mafundisho inawangusha wa Protestanti, inaonyesha kukataa kwao kwa Agano Jipya. Yesu Kristu mwenyewe anasema mfano wa kitubio. (Yoano 20,22-23): «Naye wakati alipokwisha kusema. Mupokee Roho Mtakatifu, wowote mutakayosamehe zambi, zinasamehewa, na wowote mukiwafungia zambi zinafungwa kwao vilevile». Mbele ya kusulubiwa Kwake anawaambia wanafunzi wake. (Matayo 18,18). «Kweli ninawaambia ninyi tena; vitu vyote munavyofunga duniani vitafungwa mbinguni vilevile, na vitu vyote munavyofungula duniani na mbinguni vilevile».

Ni kusema Yesu Kristu analeta neema kwa Mitume wake juu ya kuhurumia wale wanafanya kitubio. Na kama mtu anasikia mzuri hii mafundisho, ni lazima kwake kutii tu! Kwa hii mambo wakati atasikia zambi zake. Na kusema zambi zake mbele ya padri bila uwongo na woga; hivi utapata huruma ya Mungu.

Kama mtu moja atauliza, Yesu Kristu aweze kuleta huruma yeye peke yake, paka njia ya Padri? Ndiyo anaweza; lakini yeye mwenyewe anajua sababu gani alileta hii mfano. Si vema kwetu kukana hii mfano wake. Na sisi atuweze kumuonyesha yeye namna ya kupata huruma wa zambi. Sisi atuwezi kumuonyesha Yesu Kristu. «Ee Bwana aujuwe ku hurumia zambi zetu; sisi tutakuonyesha hii namna.

## 8. Ndoa

Wa Protestanti wanakataa misterio tatu: Upadirisho, Uzabitisho na Ndoa. Wao wanasema ndoa si misterio; ni unganisho tu ya mume na muke kwa kuzaa watoto. Hakuna neema hata kidogo juu yao. Ndoa haina lazima ndani ya Kanisa, ni lazima kwa wapendwa wawili kuungana mbele ya wakubwa wa serkali.

Ni huu mfano analeta Martin Luther, sababu yeye analeta mfano wake. Nao wanasema, tendo la ndoa inafanana na wanyama. Tunaandika ma sura hii: (Mwanzo 1,27-28). «Mungu akawabariki akawaambia: Muzidi kuongezeka na mujaze tena inchi na kuitiisha...». (Mwanzo 2,23-24). (Matayo 19,3-6). (Marko 10,2-9) (Yoano 2,1-11). (1 Korinto 7,10-11). (Wa Efeso 5,31-33): «Kwa sababu ya neno mume ataacha baba yake na mama yake, na atafungana na muke wake, na wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hizi ni kubwa lakini ninasema habari ya Yesu Kristu na Kanisa».

## 9.Mafuta Takatifu

Watu hawa wanakataa hii misterio wakifunga macho yao kwa hii sura na mustari wa maandiko ya Mtakatifu Mutume Yakobo 5,14-16. Ndani ya barua, Mtakatifu anaonyesha watu ya kama mmoja wao ni mgonjwa, ya fazali kuita padri wa Kanisa kumufanya sala na kumupakaa mafuta kwa mapendo ya Mungu na kwa imani ya mgonjwa, huyu atapata utakaso wa mwili na wa roho.

Tunaona ya kama hii misterio inatendeka paka kwa mpadri. Wao weko na mapokeo ya kwanza, wanaitambua ya kuwa misterio na wanaiunganisha pamoja na misterio ya kitubio. Ndani ya Agano Jipya, tuko na mafundisho juu ya hii misterio (Marko 6,13): «Wakafukuza pepo wachafu wengi, wakapakaa na mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa; wakawaponyesha». Na (Yakobo 5,13-15): «Mtu wa kwenu ameteswa? Aombe! Mtu amefurahiwa? Aimbe nyimbo. Mtu

wa kwenu akiwa na ugonjwa? Aite wazee (Wapadri) wa kanisa; nao waombe juu yake, na kumupakaa mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutaokoa mgonjwa yule, na Bwana atamusimamisha, na kama amefanya zambi, atasamehewa».

## 10.Upadirisho.

Watu wa Martin Luther wanakataa ya kama, upadirisho ni misterio. Wakati wanazungumuza, kwa makari wanasema juu ya hii misterio chuki yao, ni chuki ya Martin Luther aliyetengana na pape, aliyekana mafundisho yake, ndiyo maana aliacha kazi ya Upadri, na kubaki mwenye chuki. Kwa Wapadri wa Katholika ni kweli zamani Wapadri wa Katholika walikuwa watu wenye kutenda zambi nyingi, usharati...Ndiyo maana Martin Luther aligombanisha mafundisho ya Kanisa: Mfano misterio ya upadirisho.

Wanakataa cheo yote wa Wapadri, sababu wao wanatumainia Kanisa iko paka mbinguni. Tena wanasema ya kama waaminifu wote ni wapadri, wakionyesha sura hii: (1 Petro 2,9): «Lakini ninyi ni taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe; mupate kutangaza uzuri wake aliye waita ninyi toka giza muingie katika nuru ya ajabu». (Ufunuo 1,6): «Na kutufanya ya kuwa ufalme wa makuhani kwa Mungu na Baba yake. Kwa yeye utukufu na uwezo hata milele na milele. Amina».

Tazama namna gani wa Protestanti wote ni wa padri, ndiyo maana, haina lazima kwao kuwa na cheo ingine, paka ya Upadri. Wanaachanisha upadirisho na kazi ya Kanisa. Ni kusema upadirisho ni wa waaminifu wote na kazi ya Kanisa ni kwa watu kidogo.

Mafundisho yao nyingi inatengana na sura nyingi za Agano Jipya. Yesu Kristu anawapa Mitume nguvu, kusamehe zambi za watu, kubatiza, na kufanya misterio ingine. Kuhubiri neno la Mungu na kuimarisha Kanisa. Halafu watu walimufwata Yesu Kristu mbele na mpaka Ufufuo wake. Lakini Yeye alileta neema ya Roho Mtakatifu paka kwa Mitume wake akisema: (Yoano 20, 22-23): «Mupokee Roho Mtakatifu, wa wote mukiwasamehe zambi, zinasemehewa kwao, na wowote mukiwafungia zam,bi, zinafungwa kwao». Na (Matayo 28,19-20), na (Marko 16,14). Iko kazi wazi, Bwana Yesu mbele ya makutano analeta mupango katikati ya waaminifu. Ni kwachanisha Mitume na watu wengine, na kuwapa zawadi zake. Na hii zawadi aikuwa tu ya mwili wao, lakini ilikuwa zawadi ya kugawanya kwa waaminifu stahili juu ya kubakia ndani ya Kanisa. Nayo inaonekana hata sasa. Na kisha kupokea hii neema, siku ya kwanza Mitume walileta daraja ya upadirisho na kuacha fasi walipohubiri, wa Askofu, wa padri na Washemasi. Kwa mfano Mutume Paulo aliacha ndani ya kisanga Krete, Mtumishi wake Tito mu muji wa Efeso, mtumishi wake Timotheo. Vileviule Mitume wengine walifanya hivyo (2 Timotheo 1,6).

Mtume Paulo anashauria Timotheo kuleta zawadi kwa watu wengine, akisema kwake kufanya upadirisho kwa kila muji. (Tito 1,5) : «Na wakaweka wazee (wapadri) katika kila muji».\

Mtakatifu Ignatie, mwanafunzi wa Yoano mtume, anaandika cheo kwa wakati wake: Cheo ya Askofu, ya Padri na Shemasi. Anasema: Askofu eko pa fasi ya Kristru, Mapadri na shemasi, weko watumishi wa kazi ya Mungu. Vilevile Wapadri watakatifu walioandika mafundisho haya sawa Mtakatifu Clementi wa muji wa Roma.

Kundi chache tu ya wa Protestanti, wanasikia hii kosa yao, wakikamata cheo ya Askofu na ya Wapadri; ni kusema Arkiaskofu; na Presviteriane wao hawafwate mustari wa Mitume, na hawana Roho Mtakaitfu. Na kundi ingine ya wa Protestanti wanakataa cheo ya Padri, sababu wanatumainia wote kuwa wa kristiania na wa padri.

Na hii kosa yao, wanapokea wa mama wengine kuwa wasimamizi wa kanisa. Kwa mfano kundi moja wanaita: «Kanisa la Mitume ya Kristu». Anaweka binti wa miaka kumi na tisa kuwa musimamizi ya Kanisa lao. Mafundisho yake ya kwanza ilikuwa: «Kuvaa kanjo mufupi, kupenta midomo, kuimba na kucheza, kuvaa vyuma vya masikio».

Serkali wa inchi «Suede», mu mwezi wa kumi 1958, wanaweka dada moja kuwa pasteur (Muchungaji) na kuwa mwanafunzi wa theologia.

Na hii zoezo ilifanyika ku Kanisa la wa Protestanti, ingine katika inchi ya Danemarki, na mu Allemagne. Wanapokea barua ya Mtume Paulo ku wa 1 Korinto 14,34-35): «Wanawake wanyamaze katika ma kanisa, sababu hawana na ruhusa kusema. Lakini watu, kama sheria inavyosema vilevile....kwa sababu ni haya kwa mwanamuyke kuhubiri katika Kanisa. kama Mtume anapenda kusoma (Matendo 20,17,20, 28) . (Filiipo 1,1). (1 Timotheo 3,1-2, 3,6) . (Tito 1,7). (1 Petro 5, 1-4).

## 11. Kukataa na kuchambula uso ya Mzazi-Mungu

Kanisa Romeo-Katholika inaeshimu Mama Maria sawa Mungu sababu hana zambi, kukosa mawazo na hana zambi sawa ya watu wa kwanza Adamu na Eva, wanawapatia fazila yote. Mama Maria eko sawa wanawake wote. Hii Kanuni ilifanyika mu mwaka 1754. Lakini sisi tunajua tangu mwanzo ya kama Mama Maria ni sawa wanawake wote, sababu eko na mzazi Yoakimu na Anna, yeye anatoa roho na mwili wake kwa Mungu. Wa Protestanti wanashusha kabisa hii heshima ya mama Mzazi-Mungu. Walimupatia toka Kanisa ya Romeo-Katholika. Kwa hivi walifika kwa kumukatala Bikira Maria na wanasema Bikira alikuwa na watoto wengine. hapa wanazarau sauti ya malaika Gabrieli wakati yeye aliingia ndani ya nyumba ya Mzazi-Mungu, asema hivi: (Luka 1,31): «Tazama utapata mimba utazaa mwana utaita jina lake Yesu». Kidogo chini ya mustari 35, tunaona «Roho Mtakatifu atakuja juu yako na nguvu za Mungu aliye juu zitakutulia kivuli, kwani kile kitu kitakacho zaliwa nawe kitakuwa kitakatifu, Mwana wa Mungu». Wa Protestanti wanasema Mama Maria alikuwa na watoto wengine, hii iko wongo yao. Wale watoto ine walikuwa wa Yosefu toka bibi yake, kwa sababu, wakati alimuchukua Maria, yeye alikuwa muzee, wa padri wa kanisa wa Hebrania, walimupatia kwa Yosefu huyu Binti maria kwa kujichunga wakati alikuwa na miaka kumi na tano. Mama Maria alichunga uzima wake wa kibikira. Mbele ya kuzaa na kisha kuzaa sawa Nabii Isaya anasema: (Isaya 7,14): «Tazama Bikira atapata mimba naye atazaa mutoto mwanaume, na atamuita jina lake Emmanueli, maana la jina hili ni kusema Mungu pamoja nasi».

katika Agano Jipya ya Waevangelizaji, wote wansema Maria, mara makumi mbili na tisa: «Mama ya mtoto», kwa sababu wanataka kutuonyesha ya kama Mama Maria akukuwe Bibi wa Yosefu, mbele na kisha kuzaa Yesu. Mama Maria aliza paka Yesu Kristu kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Kwa hii mambo sisi tunamuita Theotokos, ni kusema: Mzazi-Mungu. Lakini wa Protestnanti wanakataa hii jina, lakini (Luka 1,42-43), wakati Elisabeti alijaliwa na Roho Mtakatifu, alisema: «Umebarikiwa wewe katika wanawake na uzao wa tumbo lako, umebarikiwa. Neno hili limetoka wapi? Mama ya Bwana wangu amekuja kwangu?» Katika hii siri tunasikia, Bikira Maria eko Mama Mzazi-Mungu.

Mutume Paulo kwa barua ya Waebrania (1,3) aliandika: «Yesu eko Mwana wa Mungu na barua kwa WaGalatia (4,4): «Lakini wakati ulipomalizika Mungu alituma Mwana wake aliye zaliwa na mwanamuke, ndani ya hii mistari yote, tunaona ya kama Bwana Yesu Kristu alizaliwa kwa Mungu toka kwa Mwanamuke moja ndiye Maria, njoo maana tunaita Theotokos ao Mzazi-Mungu; kwa hii mambo makutano Mkubwa ya tatu mu muji Efeso (mu mwaka 431) wanaandika fundisho ya kama Mama Mzazi-Mungu eko Theotokos, ni kusema Huyu alizala **Mungu** Yesu Kristu.

Wa ndugu wa Bwana Yesu Kristu ni hawa: Yakobo, Yosis, Simoni na Yuda walikuwa watoto wa Yosefu na bibi wa kwanza, ameitwa Maria. Kama Yesu Kristu alikuwa na ndugu zake mbele ya kusulubiwa hakupashwa kusema na Yoano asema: Tazama mama yako, lakini alipashwa kupatiamama yake na ndugu zake bila wengine.

Tunasoma kwa Muevangelizaji Matayo (28,10) ya kama Yesu Kristu siku ya Ufufuo wake alisema na wabebaji wa manukato asema: Mwende kwa wandugu zangu muwaonyesha waende Galilaya, kule wataniona. Hapa Bwana Yesu Kristu hakusema tu paka wandugu zake ine, lakini na Mitume wake.

Kisha kwa siri Matayo 13, 55: «Huyu si Mwana wa seremali Mama yake si Maria? Na ndugu zake Yakobo, Yosis, Simoni na Yuda?». Wanauliza watu wengine. Wa Protestanti wanakataa ku heshima Mzazi-Mungu ni Mtakatifu. Juu ya wongo yao wanasema wanaonyesha haki yao (1 Timotheo 2,5): «Kwa sababu Mungu ni mmoja tu, na mupatanisho katikati ya Mungu na watu ni mmoja, yule mtu ni Kristu Yesu». Hii fasi wa Protestanti wanakataa sala ya kusaidia Mzazi-Mungu. Kanisa Orthodokse anafafanisha ya kama hii chapo ao mustari imetuonyesha mapatanisho ya kama Yesu Kristu ni katikati ya Mungu na watu, lakini hii mupatanisho haina Yesu Kristu na watu. Ni kusema Mzazi-Mungu, yeye eko pa ile fasi sawa Yesu Kristu ni kipatanisho katikati ya Mungu na watu. Kanisa letu inaweka Mama Maria kuwa mupatanishi katikati ya Yesu Kristu na watu.

Kama munapenda kujifunza juu ya nini Kanisa letu Orthodoksi inaheshimu na kubusu Ikone (Picha) ya Mzazi-Mungu, mutasoma hii mustari iliyo juu na kusikia ya kama Mzazi-Mungu ni Mama ya Mungu na iko lazima kubusu Picha yake na kuomba saidio yake: (Luka 1,28, 42, 43, 48 na 11,27).

## 12. Watakatifu

Wa Protestanti wanakataa Watakatifu wote wa Kanisa ya Yesu kristu na kupokea sala zao na kukataa kuheshimu na kubusu ma picha ya Watakatifu. Ni kwa hii mambo, hawana na siku Kuu ya Watakaitfu na hawafanye sala juu ya kusaidia nia zao mbele ya Bwana Yesu Kristu.

Wanasema, sisi tunaweza kuomba mara moja kwa Mungu, bila mupatanishi katikati yetu na Mungu. Wao wanasema (1 Timoheo 2,5-6), lakini hakuna hata mukristu moja Orthodoksi anakataa hii fundisho ya Mtakatifu Paulo kwa Timotheo ya kama Mungu na watu...Sala ya Watakatifu inasaidia wokovu wa watu bila kutosha kazi ya Kristu Yesu, sawa mupatanishi. Na sisi wa Orthodoksi tunasadikia ya kama Yesu Kristu ni Mwokozi na anaunganisha Mungu na watu; na analeta amani katika ya Mungu na wanadamu.

Kazi yake sawa Mwokozi asijakuja ata Malaika ata mtu yoyote, kwa sababu paka yeye njoo alikuwa Mungu wa Mtu.

Wakati Watakatifu walikuwa hapa, waliomba kwa Mungu juu ya kusaidia wa ndugu wengine. Kwa mfano: Sawa Mtakatifu Paulo anasikia lazima ya kuomba kwa wakristu wake kwa kufanya sala juu yake; (waebrania 15,30-32).

Ndani ya hii chapita Mtume Paulo anaomba katika wa Kristu wake waokolewe toka watu wabaya wa Ebrania, kwa sababu wao wanataka ku muuwa, na kisha anaomba kwa Mungu kusudi amutembeze vizuri kwa kufika muji wa Roma.

Sura ingine inatuonyesha juu ya sisi kuomba juu ya kusaidia watu wengine ni hii. (2 Thesalonika 3,1-2), (matendo 8,24), (Wa Roma 15,30), (Wa Filipo 1,4), (Yakobo 5,16), (Ufunuo 5,8), (Ufunuo 8,3-4).

Na sasa tunauliza kama mwaminifu anaishi hapa duniani, waliomba kwa Mungu kwa kusaidia wengine, alafu kule mbinguni, awataweza kuombea wengine kisha kulala kwao?

Mutume Paulo alipiga magoti yake na kwa mapendo nyingi aliomba kusaidia waaminifu wengine. (Wa Roma 1,8-10, WaEfeso 3,14, 16, 17 na Wa Efeso 1,15). Sasa Mtume Paulo eko juu mbinguni, anacha mapendo ya kusaidia wengine wale weko hapa duniani ao Yesu Kristu anasema ya kama Mtume haweze kufanya sala? Sasa Wataaktifu, kazi yao iko paka kufanya sala; kule mbinguni juu ya kusaidia watu kibao ile wanaandika sala ya kuomba saidio ya Watakatifu.

Toka hii fundisho sisi tunasikia iko matoleo ya kweli kwa wakristu wanaomba na wanafanya sala mbele ya Mtakaitfu. Kosa ingine, wa Protestanti wanasema; Watakatifu hawajue hali ya hii dunia na hawasikie sala zetu. Fundisho yote hii iko ya uwongo; kwa sababu katika Agano Jipya Abrahamu alisema; mu kipande kwa Evangelio ya Mtume Yoano 8,56: «Baba yenu Abrahamu alifurahi kuona siku yangu; akaiona akafurahi».

Tunasikia mufano ya ule kondo aliyepotea, na Bwana Yesu Kristu alifundisha ya kama: (Luka 15, 7-10, Ufunuo 6,9-11. Ni kusema wa mashahidi wanakuwa mbele ya Mungu kwa kuhukumu watu wabaya wa dunia na Mungu anasema musiombe mbio-mbio.

Wa Protestanti wao wanasema paka Mungu njoo eko na nguvu kabisa ya kuokoa watu, na haina lazima ya Watakatifu kusaidia, lakini kazi ya wokovu sawa mwili wake, na anangaza watu wa mwili wake kwa kutusaidia kwa sala zao.

Na Mtume Paulo anasema wa malaika weko na roho ya kutumikia Mungu (Ebrania 1,14). Kama Wataaktifu na wa malaika wanafanya hii kazi, ni kusema: Wanashusha nguvu ya Mungu chini kabisa? Hapana. Wanakataa kupatia heshima watakatifu na ya Ikone yao; lakini ndani ya Biblia tuna na vitabu nyingi inasema juu ya hii mambo. (Mwanzo 18,2). Abrahamu anawabusu wageni tatu, Lota anabusu wa Malaika mbili (Mwanzo 19, 1 na 23,7, 12. Yakobo anabusu Esau Mwanzo 33,3. 6,7). Wandugu ya Yosefu wanamubusu. (Mwanzo 42,6. 43,25. 27,47 na 31,48, 12 Abrahamu anabusu Malaika (Hesabu 22,31) Yosua anabusu malaika Yosua 5,14. Lakini hii yote wa Protestanti wanakataa ikone (Picha) ya Watakatifu, katika Biblia tuko na hii fundisho. (Kutoka 25,17. Mambo ya siku 3,10...Wa Protestanti wanachunga fundisho yao ndani ya hii sura; (Kutoka 20, 4-5).

Hii fundisho iko na kazi juu ya kuchunga wa Ebrania maneno ya kufanya sanamu, lakini wasisema juu ya Ikone. Hii fundisho iko wazi kama tunaona sura ya (Kutoka 23), «Musifanye pamoja nami...» Mafundisho ingine, kuna kanuni moja 783 kisha Yesu Kristu. Ile makutano ilihukumu ile wakati watu na Wa padri kwa sababu walibusu Ikona yetu. Hii kanuni inatuonyesha hivi: «Kama waaminifu wanaona sura ya Mtakatifu, wanasikia furaha na wanapenda kufwata uzima ya huyu Mtakatifu.

Sisi waaminifu wa Orthodoksi, tunaheshimu Watakatifu, tunawabusu kwa heshima, lakini atuwabusu sawa Mungu wetu. Kwa sababu wao ni Watumishi wa Yesu Kristu. Watakatifu wetu weko na neema hii ilikuwa pamoja na Bwana Yesu Kristu, na tunaomba saidio yao kwa sababu Watakatifu ni wa rafiki na wandugu wakubusu. Sisi hatuheshimu rangi ao lubao, lakini hii heshima tunaleta inakwenda mbele ya uso ya huyu Mtakatifu.

Desturi ya zamani inatoumba na kutuonyesha ya kama Mtakatifu Evangelizaji Luka, alikuwa na moja (Agyographe) alifanya Ikone tatu ya Mzazi-Mungu na pale aliona hii Ikone alisema; Neema ya mtoto yangu na baraka yangu itakuwa ndani ya hii Ikone.

Sisi watu wote, tuna na mwili na roho, wakati tunaona ao kwangalia vitu vya kimungu (Ikone, wimbo...) inatusaidia kupandisha roho zetu mbinguni pamoja na Yesu Kristu. Na hii mambo, Ikone ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu, inafanya miujiza mingi na inatosha harufu nzuri, na inatusaidia wakati tunaomba mbele ya Ikone yao, inapashwa kwachanisha katikati ya kubusu Ikone ya Mungu na ya Watakatifu wake. Tunabusu Ikone ya Mungu ya kumwabudu na Ikone ya Watakatifu kwa heshima.

Watakatifu, Ikone yao haina sanamu. Ndani ya Agano Jipya tunasoma miujiza nyingi ya Watakatifu na Mitume wa Bwana Yesu Kristu. (Matenso 3,4-9. 5,12-16 . 9,36-41 . 19,11-12 . 20,7-12 . 28,8).

Ndani ya Biblia, sisi tunasoma ya kama Mungu anaheshimu Watakatifu wake. 1 Fal.2,30 Zaburi 4,4 Zaburi 138,17. Mezali 10,7. Ebrania 13,7). Kama Mungu anasifu Watakatifu wake, sisi tutakataa ku waheshimu? Kama Wazazi wetu ao ndugu zetu walifanya kazi mzuri, na sisi tuna na picha yao, tunaibusu na heshima, juu ya kazi waliofanya, hivi tunafanya sisi pamoja na Watakatifu wetu. Kwa sababu walituonyesha njia mzuri, na wanaacha mfano moja kwa sisi kupata uzima wa milele.

## 13. Kukataa sala ya makumbusho ya wale watu wanaisha kufariki

Wa Protestanti wanakataa sala ya makumbusho ya wafu, wanasema: Hakuna sala mbele ya Mungu ya kusaidia wale watu wenye kufariki. Kanisa ya Kristu ni yenye kuwa na vipande mbili: Ya kwanza mbinguni na ingine duniani, Kanisa ni Yesu Kristu, na anasikia sala ya watu wote wa hapa duniani na kule mbinguni kwa sababu yeye eko pahali pote. Kanisa letu Orthodoksi, hafanye sala juu ya wale weko na zambi nyingi, wakatale Kristu, lakini inafanya sala ya wale

waliishi hapa duniani katika imani, na sawa watu walikuwa na zambi kidogo, na wanakufa mbio-mbio, hawakukuwe na wakati ya kuweza kutayarisha nafsi yao.

Kanisa yetu inafanya hivi ya sala ya watu mpaka siku ya hukumu ya mwisho kuiko Yesu Kristu.

Hii sala ya kuombea ndugu wenye kufariki, tunaipata ndani ya Biblia lakini katika kitabu ya 2 Makabayo 12,40-45) (Neemia 9,1-3). Ndani ya hii fundisho wa Israeli wanafunga na kuomba Mungu, ku hurumia wazazi wao na wale watu waliofariki kwa wakati wa zamani.

Mtume Paulo ku barua ya 2 Timotheo 1,1-18, anafanya sala kwa Mungu: Bwana amupe kuona rehema kwa Bwana siku ile; ni kusema; anaomba juu ya mutumishi wake Onisiforos, Bwana Yesu Kristu alete rehema ya zambi yake ya siku za mwisho kwa sababu yeye anaisha kufa.

Jibu ingine nzuri tunabeba toka Liturgia ya Mtakatifu Yakobo na Marko, hii sala: Iko pamoja na misteri ya Komonyo, Kanisa letu inaomba neema ya huruma katika sadaka ya Bwana Yesu Kristu, juu ya wale wanaisha kufariki.

Faida gani sisi tutaombea wale watu wanesha kufa! Atujue ya kama itakuwa na namna ya kuomba juu ya wale watu weko katika gehena, kwenda mu Paradizo. Sisi atuweze kufanya sala ya wale watu walifariki bila kufanya kitubio yao; bila imani. Tunasikia vema wakati tunafanya sala ya wale wenye kufa, na wao vilevile wanasikia hii faida kwa sababu tunaungana nao pamoja katika mapendo yetu na wenye kufa. Na yote tunasikia tuna na moja Kanisa na kichwa yake ni Yesu Kristu. Mtakatifu Yoano wa Damaskinos anaandika hivi: «Mungu anapenda sisi kubeba faida yake wakati tunaishi na wakati tutakufa». Hii kazi tunafanya tunasikia ya kwanza sisi wenye, kisha na wale watu wengine.

## 14. Makosa ingine munene

Watu wa Protestanti hawasimame mpaka hapa. Wa Protestanti wengine wanaongeza makosa ingine kupita wa kuu wao, Martin Luther na Yoano Calvino. Wanakataa ya kama Biblia iliandikwa na Roho Mtakatifu, miujiza ya Yesu Kristu, na wanasema ni sauti bure. Wengine nasema Ufufuo wa Bwana Yesu haina mambo ya haki; Mwalimu Nimbhir, musaidizi mkubwa wa makutano ya ulimwengu ya Kanisa yote, anasema Yesu Kristu alifanya kosa sawa Mtume Paulo. Hawasadiki ya kama Bwana Yesu Kristu ni Mungu, lakini ni mtu wa bure.

Huyu mwalimu anasema Yesu Kristu ni Muumbaji moja wa dini tena eko mkubwa kupita wengine wa ma Kanisa. Lakini kama Bwana Yesu Kristu hana Mungu hakutakuwa namna ya kuokolewa kwa watu wa dunia.

Mwalimu wingine Bruner wa (Science) wa muji wa Zikiris anasema elimu ni yulu ya Biblia. Anaongeza tena, mtu alizaliwa toka makaka na pole-pole anageuzwa uso na mifano na anakuwa mtu. Hakuna namna ya kusema ya kama mtu eko kiumbe ya Mungu toka Adamu na Eva, hivi anasema huyu mwalimu; anasema hii fundisho ya Biblia katika kitabu ya Mwanzo inasema Mungu alifanya mtu kwa mufano wake, iko wongo? Hii fundisho iliingia katika kundi moja ya wa Protestanti inaitwa «Evangeliste», wanakataa asema roho haina ya milele, wanasema hakuna ata kitabu moja inasema ndani ya Biblia juu ya fundisho ya Roho, ya kama iko ya milele. Tena wanafunza asema hakuna gehena ya milele, hii fundisho iko mbaya na iko matushi.

Ndani ya kitabu tunasoma, tunaona ya kama wa Protestanti wote weko na kosa nyingi.

Tutasimama mpaka hapa kwa kuonyesha asema wa Protestanti weko naishi katika ngiza kwani wanakataa mafundisho yote ya Yesu Kristu alifundisha kwa neema ya Roho Mtakatifu.

Tunawatakia Bwana Yesu awaangazie akili yao kufwata Kanisa lake Orthodoksi, sababu hii Kanisa inachunga misteri yote sawa vile Yesu Kristu aliacha na Mitume wake hapa duniani.

# MAKOSA YA PENTEKOTISTE

Wakati wa Martin Luther alitoka mu Kanisa Romeo-Katholika na anafunza mafundisho nyingi, kwa mafundisho yake, kundi nyingi ya Kiprotestanti inazalikwa katika dunia mzima.

Komiti mkubwa wa Kanisa hii ni muzaliwa wa Amerika na jina lake ni Tomlinson, yeye alifanya Kanisa ya kwanza ya Pentikotiste katika muji Los Angeles ndani ya Kalifornia; paka Amerika.

Hii Kanisa inapatikana mu Grece (Hellas) katika mwaka 1918, hii kundi ni yenye kuwa na matengano na kundi ingine nyingi.

Fundisho ya Pentikotiste haina ya kwachanisha dogma ao kanuni na kundi ingine. Wa Protestanti wanasadiki ya kama Pentikotiste ni Heretique. Maneno wa Pentikotiste wanasadiki fundisho ingine ya mtu yeye peke yake anaweza kuwa na Roho Mtakatifu? Mafundisho ya Protestanti ni hii: Wanasadiki ya kama kuna ubatizo mara mbili: 1) Ya kwanza katika maji na ya pili katika Roho Mtakatifu.

2.Wanasema ya kama waaminifu wote hawana na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

3. Kama mtu anasema lugha mbali-mbali, huyu mtu eko na Roho Mtakatifu ndani yake.
4. Wanafafanusha kitabu ya uwongo ya kusema lugha nyingi kufwatana na masemo ya Nabii Yoeli na Matendo 2,17).
5. Wanafafanusha kitabu ya uwongo ya Mitume Paulo, na kusema «Wala hakuna mtu anaweza kusema, Kristu ni Bwana, ila katika Roho Mtakaitfu» (1 Korinto 12,3).
6. Wanasema tena, mambo juu ya Mtume Paulo kwa fundisho lake kwa mambo ya lugha (1 Korinto 14,1).
7. Wanafahamu matoleo ya Kanisa pa mambo ya lugha nyingi.

## Jibu ya Eklezia Orthodoksi kwa Fundisho ya Pentikotiste

Ndani ya Agano Jipya tunasoma ya kama kuiko paka ubatizo na inafika katika maji na Roho Mtakatifu. «Yesu Kristu akajibu: Kweli, kweli ninawaambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu». (Yoano 3,5) na anatuonyesha ya kama matunda kisha ubatizo ni hii: «Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaliwa kwa Roho ni Roho» (Yoano 3,6). Hapa Bwana Yesu Kristu anafundisha kwa Nikodimo ya kama wakati mtu anabatizwa anapata Roho Mtakatifu. Na kuna kwachanisha ubatizo wa maji na wa Roho Mtakatifu.

Ile siku ya Pentikote, wakati Mtume Petros alianza kufundisha, wale wa Israeli wakamuuliza: Ndugu tutafanya nini? Petrow akawaambia: Tubuni mukabatizwe kila mmoja kwa jina la Bwana Yesu Kristu, mupate maondoleo ya zambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mtakatifu (matendo 2,38).

Na hii fasi tunaona Mtume Petros anawafundisha wa Israeli ya kwamba kuiko paka ubatizo wa maji, na wa Roho Mtakatifu.

Mtume Paulo anaandika hivi kwa wa Korinto» «Kwa sababu katika roho mumoja, sisi wote tulibatizwa katika mwili mumoja, kama wa Yuda, ao wa Yunani, kama tukiwa watumwa ao wenye huru; nasi wote tumekunyweshwa katika Roho mumoja (1 Korinto 12,13).

Na Mtume Paulo anasema na watu katika Korinto wabatizwe katika maji na katika Roho Mtakatifu.

Katika barua ya Mtume Paulo (Wa Roma 8,9), anasema kama mtu moja hana na Roho Mtakatifu, huyu si mtu wake. Tena kwa barua ya kwanza kwa WaKorinto 6,19, anasema kila mwaminifu ni hekalu ya Roho Mtakatifu. «Hamujui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu? (1 Korinto 6,19).

Juu ya sisi kusadiki fundisho yao wa Pentikotiste, wanafundisha mbele ya sisi wa Orthodoksi hii kitabu ya Matendo 8,14-16) «Nao Mitume waliokuwa Yesusalema waliposikia ya

kwamba Samaria imekubali neno la Mungu, wakatuma Petro na Yoane waende kwao». Tazama, wa Pentikotiste wanafundisha na kusema ya kwamba, hawa watu walibatizwa; lakini hawakupate Roho Mtakatifu.

Mafundisho yao haina ya kweli. Yule mtu alifunza kubatiziwa ni Filipo, Shemasi toka kundi ya wale Washemasi saba, sawa shemasi, hakuna namna ya kupatia watu Neema ya Roho Mtakatifu kwa wale watu waliobatiziwa.

Mtume Paulo anaandika katika barua ya (1 Korinto 2,12) «Lakini hatupokee roho ya dunia, lakini Roho anayetoka kwa Mungu; kusudi tupate kujuwa zawadi tulizopewa na Mungu». Fasi ingine Mtume Paulo katika barua yake kwa (Wa Galatia 4,6): «Lakini kwa sababu ninyi ni wana, na Mungu alituma Roho ya Mwana wake katika mioyo yetu, anayelia; Baba, Baba».

Kufwatana na hii sura mbili tunasoma hawa waaminifu walibatiziwa lakini wanabeba Roho Mtakatifu, lakini hawa kubeba zawadi ya Roho Mtakatifu mu mifano ya kwachana, lakini hawakubeba wote mifano moja.

Fundisho ingine ya Pentikotiste iko hiyi: (Matendo 19, 1-6) Ndani ya hii kitabu watu wa Pentikotiste wanasema ya kwamba hawa watu walibatizwa pasipo kubeba Roho Mtakatifu, hivi mahubiri yao haina ya kweli kwa sababu Mtume Paulo wakati alifika mu mji wa Efeso na aliuliza wanafunzi wengine, kama walipokea Roho Mtakatifu na wanafunzi walijibu ya kama atukusikia kama Roho Mtakatifu yuko.

Walipokea ubatizo wa Yoano na Mtume Paulo anasema juu ya kusadiki na kubeba zawadi ya Roho Mtakatifu. Wakati walibatiziwa kwa jina la Bwana Yesu Kristu walibeba Roho Mtakatifu.

Ubatizo wa Yoano hauna wa kweli, ni paka ubatizo wa kutubu. Pentikotiste wanafundisha ya kwamba mtu eko na Roho Mtakatifu kama anatabiri kwa lugha nyingi.

Hii fundisho haina ya kweli, kwa sababu Mtume Paulo katika kitabu yake ya kwanza ku wa (Korinto 12,7-11), anasema hivi: «Lakini kila mtu anapewa ufunuo wa Roho ili wote wapate faida, na mwingine kufanya matendo ya uwezo; na mwingine unabii, na mwingine kutambua Roho; na mwingine namna za lugha; na mwingine kueleza maana za lugha. «Lakini kazi hii yote Roho huyu mumoja anatenda, akigawanya kila mtu peke yake kama anavyopenda».

Na fasi ingine Mtume Paulo anasema hivi (1Korinto 28,31): «Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza Mitume, wa pili Manabii, wa tatu Walimu, kisha wanafanya matendo ya uwezo, kisha zawadi za kuponyesha wagonjwa; wenye kusaidia, wenye kuongoza na namna za lugha. Wote ni Mitume? Wote ni Manabii? Wote ni Walimu wote wanatenda matendo ya uwezo? Wote wana zawadi ya kupoonyesha wagonjwa? Wote wanasema kwa lugha?...»

Ndani ya hii vitabu viwili Mtume Paulo anasema vizuri ya kwamba waminifu walibeba zawadi ya Roho Mtakatifu mifano ya kwachana. Katika Agano Jipya hakuna fasi ile inaandikwa ya kama waaminifu wote wanasema kwa lugha ya kwachana, na hi lugha ilikuwa zawadi ya ubatizo yao. Lakini kuna kitabu katika Agano Jipya inasema ya kama wale watu elfu tatu walisadiki ile siku ya Pentikosti (Matendo 9,38) Hawakubebe zawadi ya kusema lugha ya kwachana; waakti ingine watu hawakubebe zawadi ya kusema lugha ya kwachana (Matendo 4,4). Wakati alibatiziwa Towashi kwa Filipo sisi tunaona hakubebe zawadi ya lugha. Mtume Paulo alibatizwa mwanamuke Lydia bila kuandika hii jambo (Matendo 16,15), wakati Krispo mkubwa wa Sinagogi alibatiziwa hakubebe zawadi ya lugha. (Matendo 18,8), hawa watu wote tunasema hapa, walibeba Roho Mtakatifu, lakini hawakubebe zawadi ya lugha. Kwa mfano Mtume Paulo alibatiziwa na alijazwa na Roho Mtakatifu (Matendo 9,17). Lakini Paulo alijazwa na Roho Mtakatifu wakati alikuwa mbele ya mulozi Eleme (Matendo 13,9). Fasi ingine Mtume Paulo anashauria watu wakuu Efeso hivi: (Efeso 5,18). «Musilewe kwa mvinyo ndani yake ni makelele lakini mujazwe Roho...»

Pa hii fasi ingione tunasikia ubatizo ni moja haina mbili ni kusema ubatizo wa maji ni vilevile sawa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

# FUNDISHO YA WONGO YA PENTEKOTISTE

Wa Pentikotiste wanafafanua fundisho nyingi ya wongo katika Mandiko Takatifu, ndani ya hii Unabii ya Yoeli (Matendo 2,17-20). Hii Unabii, inasema; siku ya mwisho kutakuwa watu gani? Wakati Wanabii wa Agano la Kale wanasubulia mambo ya kuja kwa Bwana Yesu Kristu, ile wakati Bwana Yesu Kristu alizaliwa duniani na Unabii ingine kidogo inasema mambo ya kutimizwa kwake duniani siku ya mwisho.

Hii Unabii ya Nabii Yoeli ina na vipande viwili: Ya kwanza ni Roho inasema mambo ya kusambazwa kwa Roho Mtakatifu kwa Mitume katika juma ya Pentekosti. Na kipande ya pili inasema mambo ya ajabu itafanyika siku ya mwisho wakati Bwana Yesu Kristu atakuja kuhukumu dunia. «Jua litageuka kuwa ngiza, mwezi kuwa damu, mbele ya kutumia kwake ile siku ya Bwana iliyo kubwa yenye ajabu» (matendo 2,20). Kama Unabii moja inatimizwa isifanyike tena mara ya pili. Kwa mfano Bikira Maria anasema Nabii (Isaya 7,14): «Atazala mtoto na ataitwa Jina lake EMMANUELI». Hii Unabii ilitimizwa hakuna namna ya kufunika mara ya pili. Hivi tunaweza kusema Unabii ingine ya Nabii mu Agano la Kale. Kwa Mfano (Mika 5,2), (Yeremia 31,15), (Isaya 40,3) , (Zakaria 9,9).

Fundisho ingine ya Pentekotiste inapatikana ndani ya kitabu ya (Marko 16,17-18): «Na alama hizi zitafwatana nao wanaoamini kwa jina langu watatokeza pepo; watasema kwa lugha mpya, watashika nyoka; kama wakikunya kitu cha sumu hawatakufa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa; nao watapata afya jema».

Bwana Yesu Kristu anasema mambo haya ya alama na anasema mambo ya lugha nyingi. Sasa sisi tunauliza watu wa Pentikotiste juu ya nini wanachakula zawadi moja ya kusema lugha nyingi na wanaacha zawadi ingine ya Roho. Sisi tunasikia fundisho yao ni ya uwongo. Zawadi ya kusema lugha nyingi ni wakati wa Kanisa ya kwanza.

1).Watu wote hawana na zawadi moja ya Roho Mtakatifu. «Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza Mitume, wa pili Manabii, wa tatu walimu, kisha wanafanya matendo ya uwezo, kisha zawadi ya kuponyesha wagonjwa, wenye kusaidia, wenye kuongoza na namna za lugha. Wote ni Mitume? Wote ni Manabii? Wote ni walimu? Wote wanatenda matendo ya uwezo? Wote weko na zawadi za kuponyesha wagonjwa? Wote wanaeleza maana? (1 Korinto 12,28-30).

2). Zawadi ya kusema lugha nyingi ni zawadi ya mwisho. Kama munapenda musome katika kitabu ya (1 Korinto 12,8-10).

3). Mtume Paulo anahukumu na anachukia wale watu wanasema lugha nyingi pasipo maana. «Basi kama ikiwa Kanisa zima limekusanyika, na wote wanasema kwa lugha, na wajinga ao wale wasioamini, wanaingia, hawatasema ya kama munawazimu?» (1 Korinto 14,23).

4). Zawadi ya kusema lugha nyingi hailete wokovu, paka matunda ya Roho Mtakatifu inaokoa watu. «Kama nikisema na lugha za watu na za Malaika, lakini sina mapendo, nimekuwa kama shaba inayolia ao upepo wa kuvuma» (1 Korinto 13,1).

Na tutaandika fundisho ingine. «Wengine wataniambia siku ile: Bwana, Bwana, hatukutabiri kwa jina lako, na kwa jina lako tulitoa pepo wachafu, na kwa jina lako tulifanya matendo mengi ya uwezo? Halafu ni tawambia: Siku wajua ninyi wakati wa wote; ondokeni kwangu, ninyi munaotenda maovu (Matayo 7,22-23).

5). Zawadi ya kusema lugha, Bwana Yesu Kristu alileta ya kusaidia wa pagano (wasioamini) apana waaminifu (1 Korinto 14, 22)

6). Mtume Paulo alifahamu kusema lugha nyingi, lakini asikutumie zawadi yake. «Ninashukuru Mungu ya kuwa ninasema kwa lugha kuliko ninyi wote». Lakini katika Kanisa ninapenda kusema maneno matano kwa akili yangu nipate kufundisha wengine elfu kumi kwa lugha. (1 Korinto 14,18-19).

7). Mwalimu ni mkubwa kuliko huyu anasema lugha nyingi.(1 Korinto 14, 24-25).

8). Mapendo ni zawadi mkubwa katika zawadi zingine (1 Korinto 13,1-4).

9). Zawadi ya mwisho ni ya kusema lugha nyingi. (1 Korinto 12,30).

10). Mtume Paulo alipokea paka zawadi tatu: «Basi, sasa inadumu imani, tumaini, mapendo, hizi tatu tatu; ndiyo zawadi ya Mtume Paulo», lakini neno kubwa katikati ya maneno haya ni mapendo: (1 Korinto 13,13).

Wa Pentikotiste wanasema lugha za kwachana. Sasa tutasikia lugha gani wanasema wa Pentikotiste, watu wa kundi Pentikotiste hawaseme lugha ya kwachana, lakini wanasema maneno bila kujuwa, inaendelea toka siku ya Pentikoti ya wa Mitume. Sasa tunauliza, wa Mitume siku ya Pentikosti walisema bila kusikia ao kujuwa nini wanasema? Katika kitabu ya (Matendo 26, 12) inatuonyesha hivi: «Basi sauti hii tuliposikia, makutano walikusanyika wakafazaika, kwa sababu kila mumoja aliwasikia wakisema kwa lugha zao wenyewe».

Hapa tunasikia ya kwamba kila mtu alisikia wa Mitume kusema lugha yake. Watu wote walishangaa, wakati walisikia wa Mitume kusema lugha zao (Matendo 2,12).

Kama wa Pentekotiste wanasema lugha ya kwachana, sababu gani hawaende katika miji na kusema ao kuhubiri sawa wa Mitume wa Bwana Yesu Kristu? Kama zawadi zao ni ya kweli?

Wa Orthodoksi wanauliza: Juu ya nini waakti moja mugeni anatoka mbali na kama eko na fundisho ndani ya Kanisa yao na kuomba mtu mwingine apite mbele juu ya kufafanisha katika lugha ingine?

Na tena kama Missionari moja wa kundi la Pentikotiste anataka kwenda fasi ingine, inafaa kwanza kufunza lugha ya ile mugini ataenda?

Sasa wa Mitume wa Bwana Yesu Kristu walikuwa lazima na mtu juu ya kufafanisha mafundisho yao?

Watu wote wanafwata fundisho ya kundi ya Pentekoti wanasikia ya kama lugha yao haina na maana na iko sawa lugha ya Babylone. «Watu wa kundi ya Pentikotiste weko na pepo ya kulakuisha, pepo ya nyoka». Namna gani sisi wa Orthodoksi tutaweza kufafanusha hii neno ya lugha pasipo maana ya kufafanusha hii lugha ya mugeni waakti wa kuhubiri ndani ya Kanisa yao? Hii jibu tutabeba toka sauti ya Mungu katika Biblia Takatifu.

Shetani ni mkubwa ya uwongo. Shetani kama anataka kundi kuyafanya sawa Mtume wa Mungu. Nabii wa Mungu, Mutumishi wa Mungu na tena Malaika wa Nuru. Mambo munene ni kama shetani anakuja mu dunia sawa Yesu Kristu, lakini huyu eko Antikristu.

Mtume Paulo anasema katrika barua yake kwa wa 2 Korinto 11,13-15): «Maana hawa ni Mitume ya uwongo, wenye kutenda kazi kwa hila, wakijigeuza wenyewe kuwa kama Mitume ya Yesu Kristu. Wala si ajabu; kwa sababu shetani mwenyewe anajigeuza awe Malaika wa Nuru. Basi ni neno kubwa kama watumishi wake vilevile wanajigeuza wawe watumishi wa haki, mwisho wao utakuwa sawa sawa na kazi yao».

Tena huyu shetani anajifanya kuwa mwalimu wa Evangelio. Sauti ya Mungu inasema hivi: «Ikakuwa tulipokwenda kuomba, tukakutana na kijakazi mwenye pepo ya kwanguka. Naye alipatia Bwana Yesu faida zake nyingi kwa kutabiri; yule alifwata Paulo, na sisi, akapaza sauti, akilia: Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kutuhubiri njia ya wokovu. Akafanya hivi kwa siku nyingi, lakini Paulo alihuzunika.

Naye akatoka kwake saa ileile» (Matendo 16,16-18).

Hapa tunaona shetani alitumia ule binti sawa mujimbe wake juu ya kuonyesha watu wengine kufika kwa Bwana Yesu Kristu. Watu wa Pentekotisti weko na pepo ya nyoka (ao ya kuanguka). Na kwa hii mambo ya wale watu wanasema lugha nyingi na wale wanasikia haina na maana. Haina zawadi toka Roho Mtakatifu kwa sababu hii tendo tunaiona ndani ya Kanisa ingine.

Sasa tunauliza iko namna ya kupata Roho Mtakatifu ya Mungu ndani ya Kanisa nyingi? Hapana kwa sababu Mtume Paulo anasema: «Bwana mmoja, imani moja, ubatizo...» (Efeso 4,5). Sasa sisi wote tunasikia hii pepo yao haina Roho ya Mungu, iko roho ingine. Evangelizaji Yoano katika barua yake ya kwanza, sura 4,1, anasema hivi: «Wapenzi, musiamini kila roho, lakini jaribuni roho, kama zimetoka kwa Mungu; kwa sababu manabii ya uwongo wengi wametokea

duniani». Kama kundi ya Pentekotiste walikuwa na roho ya kweli iliwapaswa kwenda fasi ingine dunia nzima, sawa vile wa Mitume wa Bwana Yesu Kristu, juu ya kuongoza watu njia ya Paradizo. Haina hivi kwa sababu kundi yao, hakuna umoja, kwa lakini iko nyingi na kundi yote iko karibu makumi mbili na tano.

Kundi moja ingine inahukumu kundi ingine, inasema kundi yangu ni ya kweli na ingine haina ya kweli weko wa heretique.

Toka hapa tunaona kama Roho ya Mungu haitumikake ndani yao, kwa sababu Roho ya kweli inaungana na watu na inaleta amani, mapendo katikati yao, wema na furaha.

## MATOLEO YA KANISA YA KWANZA

Hii zawadi ya kusema kwa lugha inaonekana wakati wa Mitume, waliishi na hii zawadi iliisha kuisha juu ya nini?

Jibu inaleta na Yoano Krisostomo: «Zawadi ya Roho ya Mungu ilikuwa lazima ile wakati kwa sababu Kanisa alifanya mwenendo wake wa kwanza. Ile wakati Kanisa ilianzia kukombanisha adui zake mbili, mkubwa wa kwanza ni wa dini ya Ebrania na wa pili watu wapagano.

Kristianisme asiweze kukombanisha mambo ingine na kundi yake ilikuwa ya kuhubiri Msalaba na Ufufuo wa Bwana Yesu Kristu, ilipaswa Mungu kuonyesha nguvu yake ya Roho Mtakatifu mbele ya wale watu waliisha kwa ile wakati. Na hii mambo aliwapatia wale watu zawadi ya Roho Mtakatifu juu ya kusikia nguvu ya imani yao mpya.

Hadizi ya Kanisa na matoleo yake hayandike ya kama ni zawadi ya kusema lugha nyingi sawa wakati wa Mitume, kwa hii waakti ilishimamishwa. Hii zawadi ilishimamishwa ya kwanza, zawadi ingine ilianza kusimama pole-pole, lakini hapana yote. Sasa sisi tuna na lazima ya imani, hapana ya alama. «Heri wale wasioona, lakini wameamini». (Yoano 20, 29).

Na sasa Roho Mtakatifu anafanya miujiza na alama ingine ya kuponyesha watu wagonjwa, lakini mihujiza munene kupita iko; wakati moja mtu fulani ataacha njia ya ubaya ataamini kwa Mungu, atatubu na ataweka ndani ya roho yake neema ya Roho Mtakatifu.

## Kundi ya Pentekotiste ni wa Heretique

Sisi tunajua ya kama mbele ya Bwana Yesu Kristu kupanda mbinguni alipatia wa Mitume wake Roho Mtakatifu. Wa Mitume wake wanafanya upadirisho na wanafunzi wao. Na hii mustari yao ilifika na mpaka sasa. Kanisa yetu Orthodoksi iko na cheo yote ya upadirisho. Wa Askofu wa kanisa letu wanaleta Roho Mtakatifu tokea Bwana Yesu Kristu na Mitume wake.

Kundi ya Pentikotiste wanachagua ndani ya kundi ya waaminifu wao, kwa sababu wanakataa cheo yote ya upadirisho. Wanakataa ma Fumbo yote ya kanisa ya Yesu Kristu. Na kabisa Fumbo ya Komonyo na Maugamo.

Wanakataa Matoleo ya Kanisa ya kweli na wanazarau fundisho ya Mtume Paulo ya kusema (2 Thes. 2,15): «Basi, ndugu, simameni kwa nguvu mushike mafundisho muliofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa Bwana wetu».

Wanakataa Mama Maria ya kama ni Bikira mbele ya kuzala na kisha kuzala yeye alibakia paka Bikira. Wanakataa sala ya kuomba Watakatifu mbele ya Mungu juu ya wokovu wetu.

Sisi tunapenda kundi ya Pentikotiste na tunafanya sala juu ya Mungu kufungula akili yao ya kurudia mu Kanisa ya kweli Orthodoksi; sisi waaminifu wa Orthodoksi haina na faida kwenda Kanisa yao ao na kusikia fundisho yao, kwa sababu kundi yao ni inje ya Kanisa wetu wa kweli.

# Jamaa ya Methodiste

Mwanzo ya kundi Methodiste inatokea kwa walimu na wanafunzi wa moja wa muji Oksfordi ya inchi Anglia. Ile kundi ilikuja duniani mu mwaka 1728 na mkubwa wao jina lake Yoano Weslei. Huyu mkubwa pamoja na ndugu na rafiki zake waliandika mustari moja kwa kufanya kazi ya Mungu.

1) Wanaongeza saa nyingi juu ya kusoma Madiko Takatifu.
2) Wanasikilizana juu ya kutembelea watu wagonjwa.
3) Wanafanya mafungo mu kazi tatu na mu kazi tano.
4) Wanatayarisha siku ya kukamama Komonyo Takatifu.

Na mu mwaka 1738 hii kundi ilikuwa na watumishi wengi; na fasi yao, mkubwa yao wa kazi alikuwa mu muji wa Londres. Na kisha walitembea mu muji ingine nyingi.

Yule mkubwa yao Weslei alikuwa tena Padri mu Kanisa Anglikane. Huyu mtu njoo alifanya kundi ya Jamaa la Methodiste mu mwaka 1738.

Mwanzo wa mwendo wake alifanya nyumba juu ya kufanyizia fundisho na sala; lakini pasipo baraka ya Kanisa lake. Huyu mkubwa alichakula watu wa pagano na kuwaweka wakubwa ama wachungaji bila upadirisho na askofu yao. na hii kazi alifanya mu safari yake ya pili; na iliachanishwa na kanuni ya kanisa lake.

**<u>Safari ya tatu ni hii:</u>**

Padri Yoano Weslei bila baraka ya askofu wake alibadirisha wachungaji mbili (waaskofu) mu tarehe 2-9-1784 na aliwatuma sawa wakubwa wa Missionnaire wa inchi Amerika.

Safari ya ine na ya mwisho ya mashindano yake ilifanyika mu mwaka 1786. Padri mkubwa alikamata kitabu ya Euchologie mkubwa ya Kanisa ya Anglikane; juu ya kusoma sala bila baraka ya kanisa lake. Kisha wakati ndogo wahubiri wake wakakula Komonyo, bila baraka ya padri mkubwa (Yoano Weslei) yao.

Na huyu mkubwa wao akawafukuza; lakini wahubiri wake wakaendelesha kazi yao, bila ruhusa ya mkubwa yao.

Na wakati ule mkubwa alikufa,mu mwaka na tarehe 2-3-1791 na kundi ilikuwa nyingi. Mu mwaka 1793 wahubiri wote wakakusanyika na wakaleta kanuni ifwatayo:

Imekatazwa kula Komonyo bila baraka ya wakubwa wao; na hii sala ya komonyo iko na namna ya kuyafanya mpaka mujuma mangaribi.

Mu mwaka 1794, waliandika fundisho ya ubatizo wakasema:

-Kundi inapaswa kusikilizana mbele ya kufanya ubatizo. Na hii misteri yote mbili wale wanapashwa kufanya ni paka kundi inaleta ruhusa ya kutenda ile kazi. Na kuomba ruhusa ya kufanya na saa ya kuhubiri.

Tangu mwaka 1797 kukatokea vipande vingine vya kundi na wingi wa wote ni 12 kufika mpaka mwaka 1932.

Kundi ya Methodiste inaisha kuzambalala katika dunia nzima. Ya kwanza iko ku kisanga ya Irland na mu inchi Amerika.

Siku moja mkubwa Yoano Weslei akamuomba Askofu wa muji London juu ya kufanya upadirisho ya wa padri, lakini askofu wa ile inchi akakatala kuleta ruhusa; kisha mkubwa akafanya upadirisho bila ruhusa ya Mapadri na kuwatuma ku inchi Amerika na kule ma kundi yote iko 30.

Wakati Yoano Weslei aliisha kundi lake ilikuwa na mashindano hii:

1)Makusanyo munene wa ma kundi mara moja pa juma,
2)Kila mtu anapashwa kufika na wakati kila juma bila ku kosa.
3)Sala inapashwa kusemwa mbele ya kufanya kila fundisho.

4) Wote watasumbulia kweli na kufatana moja kwa moja na watasema zambi zao katikati yao na kisha wataomba shaurio na saidio ya majaribu yao yote;
5) Na kati yao kutakuwa muongozaji moja na yeye atauliza wale waliosema zambi zao hivi:
   a) Majaribu gani munapata ku hii wakati wote?
   b) Nani alifanya zambi mu makutano ya zamani paka ya sasa?
   c) Namna gani munakombana na hii majaribu?
   d) Mazungumuzo gani munafanya ku hii wakati munazungumuza mambo moja mbaya?

Kama kundi ni munene wanachakula mchungaji (pasteur) moja na mpaka ni tano, na watu wengine wakuhubiri; watawa ao Laics. Na huyu mchungaji atatumika yeye peke mu amri wa miaka mbili na kisha, wanamuweka fasi ingine.

Na wale watawa waliochakuliwa watatumika ile fasi na mpaka uzima wao wote. Na hawa wa kundi lote weko na Askofu; hii kundi ya Laics na mchungaji wanachakula makutano ya askofu. Hii yote askofu hana na uriti wa upadirisho wa kweli hawana na Roho Mtakatifu ndani yao. Na kazi ya kila askofu ni juu ya kuchakula mchungaji na wahubiri wa kubakia mu kila parokia yao.

## Fundisho yao ya uwongo

Na mafundisho ya hawa watu ni pamoja na makundi ingine, lakini fundisho yao iko hivi:
a) Paka Madiko Takatifu iko na fundisho yote juu ya kusaidia sisi kupata wokovu.
b) Hakuna imani nyingi mu mambo ya Utatu Mtakatifu na hakuna nguvu ndani yake.
c) Wanakatala misteri yote ya Yesu Kristu, lakini wanaamini kabisa ya upadirisho na weko nafanya ubatizo na komonyo sawa alama, lakini bila kusadiki kunatoka hii kuna samna ya kuokolewa kwa neema ya Roho Mtakatifu. Na hawasadiki ya kama Mama Mzazi-Mungu ni Bikira kamili. Hakuna heshima juu ya sala ya Watakatifu wa Bwana Yesu Kristu.

Wa Protestanti wote wanasadiki ya kama wokovu ni namna ya kupata imani. Kundi ya Methodiste ni munene mu dunia mzima. Mu Afrika ni kundi moja katikati ya Methodiste na jina lake ni «Orthodokse Apostolike Kanisa ya Afrika». Hii kundi haina ndani ya Kanisa yetu Orthodoksi; iko ya kukokota waKristu wa Kanisa yetu Orthodoksi.

## Jamaa ya Evangeliste

Jina yao ni Evangeliste ao Presviterien, kwa sababu wanachunga cheo ya upadri na wanafukuza ile askofu na shemasi na mkubwa yao ni bwana Yoano Calvinos. Hii kundi inazalikwa mu inchi Aglia mu kipindi kimoja kinaitwa Skotia; njoo mwanzo wa Kanisa ya Skotia. Na inchi ya Skotia inafuchika ile Kanisa na kusaidia sawa ya serkali yao.

Fundisho yake iliandikwa kwa mwanafunzi moja na jina lake Yoano- Noks mu mwaka 1560. Mu ile Kanisa ya Skotia munesha tokea tena kundi ingine tangu mwaka 1746; na jina ya ile kundi ni Voulgerie.

Mu mwaka 1843 kundi ingine moja ilizalikwa na jina : «Kanisa ya Uhuru». Hii vipande ya kundi, inagawanika sababu kundi la Skotia iko nafwata paka kanuni ya serkali yao.

Na kisha mwaka moja, watu walianza kutoka mu kundi ya Skotia. Hii Kanisa yao inafwata fundisho ya Yoano Calvino; na walichana na kanisa ya Anglia mu mwaka 1572.

**Fundisho ya Yoano Calvino**

a)Mungu ni Mwogozi wa dunia nzima.
b) Mtu ana na uhuru wa kufanya kazi yake ni paka kuomba Mungu awaongoze wote na kuleta ruhusa ku mashindano yote.

c) Paka Yesu Kristu eko na uwezo wa kuleta matunda ya wokovu hapana mutu yeye mwenyewe.
d) Bwana Yesu Kristu alisulubiwa paka juu ya watu wazuri hapana juu watu wabaya.
e) Wokovu ni paka ya wale watu Bwana Yesu Kristu anesha kuchagua.
f) Neema ya Roho Mtakatifu itafika paka kwa watu walio chakuliwa; hata kama watu hawana na lazima, lakini kwa nguvu neema itawafikia kwao.
g) Wale watu waliochakuliwa; watabaki karibu ya Mungu mpaka milele.

Hii fundisho yote ya Yoano Calvino iko na kosa; Mungu anaumba mtu na uhuru wake mwenyewe na tunaona Bwana Yesu Kristu alifika mu dunia; si juu ya watu wa haki, lakini juu ya watu wenye zambi wa wokolewe mu vitendo vyao mbaya. Na Bwana Yesu Kristu anatufundisha ya kama; mtu akitaka kunifwata achukuwe Msalaba wake na anifwate, lakini Yoano Calvino yeye anasukuma mtu bila ku mu heshimu.

Kundi ya Presviterien iko 35 mu dunia mzima; na mu hii kundi kila wakati munatoka vipande vya kwachana maneno ya makosa nyingi.

## Jamaa ya Kanisa Catholike Apostolike

Mwanzo wa kundi yao ni mu mwaka 183) mu London na mkubwa yao ni mchungaji Irving. Watu wa hii kundi wanasadiki ya kama iko ya kweli mu dunia mzima, na wanasema hii kundi yao ina zawadi ya Roho Mtakatifu. Na wanaongeza ya kwamba Roho Mtakatifu analeta neema ya kuchakula wakubwa wote wa kanisa yao. Sawa Mitume 12, Prophete na Askofu na mapadri zao.

Fundisho yao ingine wanasema hivi: Roho Mtakatifu hachague wa Diacres saba, ile tunasikia katika kitabu ya Matendo ya Mitume, lakini ni kundi inakusanyika kwa kuchagua wa Shemasi.

Kazi ya kundi yao inaomba ma kundi yote kurudia mu Kanuni ya kale; maneno wanapoteza mifano yao ya zamani. Kanisa yao ingine ilifika mu Amerika mu mwaka 1851; na Mtume yao wa mwisho alifariki mu tarehe 1901. Tangu hii wakati cheo ya padri ilikuwa kidogo; kwa sababu walianza kuongojea paka siku ile Mungu atachagua kidogo; kwa sababu walianza kuongojea paka siku ile Mungu atachagua Mitume wengine. Naa kisha mwaka 1860 kipande ya kundi inatoka juu wanakataa kuweka pa fasi ya Mtume mwenye kufariki mtu mwingine; na kipande ile iliotoka jina ni «Neo Apostolique» nikusema: «Mitume Wapya». Hii kundi yote mbili Mitume Wapya na Kanisa Katholike wote wanatenda kazi moja mu kundi yao.

## Jamaa Adventiste

Jina yao ingine si Sabatiste kwa sababu wanaheshimia siku ya saba, ni kusema mu posho; ni mufano moja na wa ndugu Waebrania kule inchi ya Israeli na hii mambo inapatikana katika Agano la Kale. Mkubwa yao jina lake Gulielmos Miller. Na aliishi mu inchi ya Amerika mu mwaka 1772, na kazi yake ni mashamba. Lakini fundisho yake ilianza mu mwaka 1831. Mahubiri yake iko hivi: Mafundisho ya Prophete Danieli na mwevangelisti baba Yoane juu ya mambo ya Ufunuo ni kusema; maneno ya mwisho ya dunia, Miller anasema hii habari inafika mu dunia mu mwaka 1843; mwezi wa tatu tarehe makumi mbili na moja ya mwaka uo, Mwana wa Mungu atashuka katika mawingu kwa nguvu na kwa Utukufu nyingi. Na kisha watu wengi waliacha kundi yao na kumufwata; juu ya kuonjea waakti ile ya mwisho.

Na siku ile alisema ilipita na hakukuwe mambo ata moja. Watu wote wakasikitika na Miller akasema Watumihsi wake walifanya kosa kwa kuhesabia masiku. Kisha akawaonyesha watu tarehe ingine ya uwongo; asema Bwana atafika mu mwaka wa 1844, mwezi ya kumi siku

ya makumi mbili na mbili, lakini ile siku ilipita hakukufanyike kitu ata moja; wote wakaona udanganyifu wa ule mwalimu.

Kisha akaacha kufundisha na kuhesabu masiku ya kuja kwa Bwana Yesu Kristu mu dunia. Na kundi ingine ikatoka mu mwaka 1846. Na mu mwaka ingine mu kundi nyingi ikatoka yote, na wingi wa ile kundi ilikuwa kumi na tatu. Kazi yao walileta saa nyingi juu ya kusoma na kufundisha Agano la kale na ile yote ilikuwa kwa akili na kwa mapenzi yao, lakini namna ya kufafanusha wote walikuwa wanaachana. Na walikuwa na mchungaji juu ya kufanya sala na wote hawakuwasadiki zaidi misteri ya upadirisho. Wanapokea ubatizo na Komonyo sawa alama apana sawa misteri ya Bwana Yesu Kristu.

## Jamaa ya Adventist ya siku ya Saba

Mkubwa ya hii Kundi alikuwa mama Heleni Gouaite. Fundisho yake iko hivi: Anasema Yesu Kristu alikuja mu mwaka 1844, na kazi yake ilikuwa juu ya kusafisha Altare ya mbinguni kule walienda pamoja na mama Heleni naye aliona hii mambo yote.

Fundisho yake ni hii:

1) Hasisadiki ya kama Bwana Yesu Kristu eko Mungu na kwa Utatu Mutakatifu na anaongeza ya kwamba Yesu kristu eko mtu wa zambi sawa watu wote.
2) Hapana kupokea Kanisa ya Yesu Kristu.
3) Kwao wanapokea Ufalme wa kimtu ao wa ki binadamu. Na kisha wanafafanusha mambo ya uwongo na mbaya.
4) Kwa watu wale hawataokolewa watapotea kwa sababu hakuna gehena ya milele kwa hii maana yote itapotea.

Wakati Bwana atafika mu dunia paka 144.000 watu watafufuka na watapanda pamoja naye; na watabaki pamoja na Bwana Yesu Kristu miaka elfu.

Hii wakati wote dunia itakuwa gerezani ya shetani na kisha miaka elfu Yesu Kristu atakuja mara ya pili kuhukumu watu; wakati watu wa zambi watapotea, dunia itasafishwa kwa moto na wale wachakuliwa watashuka pamoja na miili zai kwa kuishi bila lazima ya vitu ya chakula.

Fundisho yao inafwata na fundisho ya Yehova. Na hii yote iko ya uwongo kabisa kwa sababu inaachana na ya Yesu Kristu, na ya mu Biblia. Mu dunia yote numero ya kundi Adventist, nikusema wingi wao weko 1.500.000 watu lakini mu inchi Amerika wote weko 300.000 watu.

## Tabernacle

Hii Jamaa ilitoka ku Jamaa ya Pentikotiste mu 1933. Ilifika hapa kolwezi ya Kongo mu mwaka 1978 na ina waaminifu 2000. Jina Tabernacle ni ya lugha kifransa maana ya hii jina inaonyesha «Nyumba ya Mungu». Prophete wao alikuwa jina lake William Marrio Branham; alikufa mu 1965. Sasa hawana na Propheta watachagua mwingine siku za mbele.

Wanasadiki ya kama Kanisa yao inatoka katika Yesuralema ku kanisa ya kwanza. Wao wanasema Kanisa ya Yerusalema ilibaki ya kweli mpaka mwaka 325. Kisha walipoteza uhaki wa Bwana Yesu Kristu. Lakini na hapa sasa hakuna Kanisa ya kwanza. Hii mafundisho yao ni ya uwongo kwa sababu Bwana Yesu Kristu anasema kwa Kanisa yake «Wala milango ya Hadeze haitalishinda». (Matayo 16,18).

Bwana Yesu Kristu atabaki mkubwa wa kanisa yake milele na milele» (Matayo 28,20). Kanisa ni mwili wa Bwana Yesu Kristu na huyu ni kichwa yake. (Wa Efeso 1,22-23). Bwana Yesu Kristu ni mwenye nguvu kupiota shetani; lakini hakuna namna ya kwanguka Kanisa lake na kupoteza kazi yake: (1 Yoano 4,4). Roho Mtakatifu inaongoza Kanisa ya Bwana Yesu Kristu (Yoano 14, 16-17); inaongoza ukweli wa mafundisho yote (1 Yoano 16, 13).

Kanisa ni nguzo (colone) na msingi wa kweli (1 Timotheo 3,15).
Wa Tabernacle wanasema ya kama kanisa Catholike pamoja na mkubwa yao pape walianguka katika mafundisho ya uwongo. Na hii kanisa Katholike ilitoka katika Kanisa Orthodokse, lakini hii Kanisa inaharabika na inapoteza neema ya Mungu. Hawa wandugu zetu hawajui Hadizi ya kweli ya Kanisa ya Bwana Yesu Kristu. Halafu inapashwa kufunza na kujua ya kama Kanisa Katholike ilitoka ku Kanisa ya kwanza ya Bwana Yesu Kristu mu mwaka 1054, na kweli ilianguka katika makosa nyingi kwa sababu iliweka sawa kichwa yake mtu moja aliye Pape. Lakini Pape anasema Yesu Kristu ni mkubwa paka wa kanisa yake ya mbinguni. Kanisa ya kwanza kufika mwaka 1054 iliitwa Kristianisme na ni moja tu duniani. Leo hii Kanisa inaitwa Orthodokse (Fundisho ukweli). Inachunga mafumbo yote na Kanuni za mafundisho ya wa Padri Watakatifu; bila kosa hata moja. Hii Kanisa iko kweli na Roho Mtakatifu, inatakasa na kuokoa watu. Alama moja mkubwa ni kwa sababu miili ya Watakatifu wetu inabaki mzima, bila kuoza na inatoa harufu nzuri na inafanya miujiza nyingi.

Waaminifu wa Kanisa Tabernacle wanakataa Utatu Mutakatifu na wanapokea uso moja ni paka Bwana Yesu kristu. tena wanasadiki ya kama Mungu huyu anageuza uso wake na wakati ingine inaonekana sawa Baba nma wakati ingine sawa Bwana Yesu Kristu na wakati ingine sawa Roho Mtakatifu.

Kama wa ndugu zetu wa Tabernacle wanapenda wokovu wao ni lazima kufungua akili na masikio yao kwa kuangalia mafundisho ya kweli ya Biblia Takatifu.

Mungu ana uso tatu ya kuachana katikati yao. Hii ni Misterio hakuna namna ya sisi kufafanusha kwa akili yetu. Paka kwa imani ni namna kuipokelea. Agano la Kale (Mwanzo 1,26) inasema hivi: «Tufanye mtu kwa mfano wetu, wenye sura yetu».

Hii sura inatuonyesha ya kama haina paka moja, iko tena na ingine. Vile inapashwa kusikia na mistari ingine (Mwanzo 3,22 . 11, 6-9) Nabii Isaya 6,3) anasema mara tatu jina la Mungu Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu. Abrahamu alipokea wanaume tatu, hawa wanaume walikuwa malaika, lakini ni alama ya uso tatu ya Utatu Mutakatifu.

Hapa wa Tabernacle wanaleta ufafanusho wao. Wanasema mwanume moja alikuwa ni Yesu Kristu na wengine wawili weko wafwasi wake. Sisi tunawauliza ya kama namna gani walijua ya kwamba mwanaume moja ni Bwana Yesu Kristu, na haw awawili ni kundi lake? Ni vile Biblia Takatifu inasema? (Mwanzo 19,24): «Halafu Bwana akanyesha juu ya Sodoma na Gomora kiberiti na mto toka Bwana mbinguni). Sisi tunawauliza: Bwana moja ni Bwana Yesu Kristu, sasa wale wawili ni wa nani? (Isaya 59, 15-20). Hapa tunasikia ya kama Nabii anatuonyesha ma uso tatu ya Mungu (mustari 19-20).

Hapa Bwana (Yesu Kristu) kwa kinywa ya Nabii anasema: Bwana (Baba Mungu) alinituma mimi (na Roho ya Bwana). Tunaona ya kama haina uso moja ya Mungu lakini ni ma uso tatu ya Utatu Mtakatifu.

Tunaona na kusikia vizuri hii jambo katika vitabu vya Agano Jipya. Kwa mfano waakti Bwana Yesu Kristu alibatizwa katika mtoni Yorodani (Matayo 3,16-17). Wakati alituma Wanafunzi wake kuhubiri habari njema (Matayo 28, 19); wakati Mtume Paulo alionyesha wa Kristiani wengine kwa kumuweka katika sala yao (Wa Roma 15,30), wakati huyu Mtume alitakia wa Kristiani wa Korinto baraka ya Utatu Mtakatifu kuwafisha (2 Korinto 13, 14).

Tunaona mara ingine hii mafundisho ya Mtume Paulo (Wa Galatia 4,6) na (1 Korinto 12, 3-11). Tunakuwa tu wafupi kwani mafundisho iko nyingi ndani ya Biblia Takatifu; sasa tunaandika hii ma sura kidogo ya kumisaidia ninyi wa ndugu.

Sawa vile wa Protestanti na wa Tabernavle wanakataa ya kama mama Mzazi-Mungu ni Bikira katika uzima wake. Wanasimamia katika kitabu ya Matayo 13, 55-56 na Luka 8, 19. Hii mistari ya Matayo na Luka inatuonyesha ya kama hii ni mawazo ya wa Ebrania, nao hawakufahamu ya kuwa katikati yao alifika Mungu na Mwokozi wa dunia ndiye Bwana Yesu Kristu. Mama Mzazi-Mungu anasema katika kitabu ya Luka 1,34, anasema» «mimi sijue mume». Hawa watoto ine Yakobo, Yosis, Simoni na Yuda walikuwa watoto wa Yosefu na bibi yake, aliyeisha kufa. Mama Maria hakuwa bibi yake, lakini alikuwa mchumba yake na Yosefu alikuwa

mlinzi na mchungaji wake (Luka 2,5 . Matayo 1, 18-20). Vile inasema Agano Jipya Yosefu ni mwenye haki; na wakati alimubeba Mama Mzazi-Mungu alikuwa na umri wa miaka 15 ama kumi na tano. Hapa tunauliza ya kama Mama Maria alikuwa na miaka 15, watoto wa Yosefu walikuwa wakubwa kwa sababu Baba yao alikuwa muzee. Sisi wa Orthodoksi tunauliza Mama Maria alikuwa na miaka 15, namna gani alipashwa kuzala watoto wa kubwa wa miaka 30 na 40 miaka? Vile sisi tunawaza (Matayo 2,14) hii verset inasema ya kama Yosefu alichukua mtoto na Mama yake kwenda mu Misri. Hasiseme mtoto na bibi yake! Mama Mzazi-Mungu alikuwa Bikira katika uzima wake ni kwa hii mambo anasema kila kizazi ya watu watamutukuza (Luka 1,48-49).

Wa Tabernacle wao wanapenda kuwowa wanawake wengi (Polygamie) « Nyumba na mali ni uriti unatoka kwa Baba: lakini muke wa akli anatoka kwa bwana.(Mezali 19,14). Mtume Paulo anasema ku (1 Korinto 7,10-11): «Muke hawezi kwachana na mume wake. Maungano ya mume na muke ni alama ya maungano ya Bwana Yesu Kristu pamoja na Kanisa lake. Bwana Yesu Kristu hawezi kuwa na ma Kanisa nyingi, kwa sababu yeye ni kichwa ya Kanisa moja.

Walimu wa Tabernacle wao wansema sisi tuko Watakatifu tutaenda mu Paradizo. Sisi tunawatakia wote kwenda katika Paradizo, lakini musome» «Tunawauliza ya kama munafanya utii wa kitabu ya Yakobo» (Yakobo 1,22).

Wanachunga matoleo anasema Mtume Paulo katika kitabu ya (1 Korinto 11, 1-2), (2 Thesalonika 2,15 na 3,6) , (2 Timotheo 1,13-14) , (2 Timotheo 2, 1-2). Weko na unyenyekevu ya Mtume Paulo: (Wa Roma 5,8. I Korinto 4, 9-13; 15, 8-9) Wanafahamu ya kwamba haina imani ya wokovu? (Yakobo 2,17-26). Munajua uzima wenu utakuwa wapi kama munazarau amri ya Bwana Yesu kristu? (Matayo 5,19; 7,21-27)? Munabeba mwili na damu ya Bwana Yesu Kristu kwa kupata uzima wa milele? (Yoano 6, 53-54; 1 Yoano 1,7; Matayo 26, 26-28; 1 Petro 1, 18-21; Efeso 1, 7)?
Kama wanasadiki ya kama ni watu wa zambi wanatubu kwa zambi zao? (wa Roma 3,23; Matayo 3,2 na Luka 13,13).

Wanakataa Msalaba wa Bwana yesu kristu, lakini alama ya msalaba sisi tunaipata katika Agano la kale. Abrahamu alibariki watoto wake kwa alama ya Msalaba kwa mkono wake (Mwanzo 48, 13-15). Ssisi wa Orthodoksi tunaabudu Bwana Yesu Kristu na tunasifu alama ya Msalaba wake. (2 Wafalme 18,4). Wakati wa Israeli waliaabudu ule nyoka ya shaba swa Mungu, mfalme Hezekia alibomoa ule nyoka ya shaba.

Bwana Yesu kristu alitukuzwa katika Msalaba wake (Yoano 12,16; 12,31 na Filipo 2, 9-10). Msalaba ni wokovu wa waaminifu na upumbafu wa watu wenye kupotea. (1 Korinto 1,18-21). Maadui wa Msalaba wa Bwana Yesu Kristu watapotea: (Filipo 3,18-19; Wa galatia 6,12). Msalaba ni utukufu wa Mtume Paulo: (Wa Galatia 6,14). Katika Msalaba watu walisamehewa zambi zao: (Kolosayi 2,14-15). Msalaba unaleta amani katikati ya Mungu na watu wote: (Wa Efeso 2,16; Kolosayi 1,20). Msalaba ni silaha mbele ya shetani. Sisi wa Orthodoksi tunasifu Msalaba wa Bwana Yesu Kristu hapana sawa ubao bure, lakini sawa alama ya sadaka ya Bwana Yesu Kristu. Kama tunasifu Msalaba ni vilevile tunasifu Bwana Yesu Kristu. (Zaburi 131,7).

Wokovu na utakaso wa roho si vitu teketeke watakatifu wote kwa mateso na sikitiko nyingi waliingia katika ufalme wa mbinguni (Matendo 14,22 na Kolosayi 1,24). Wanafanya uvumilivu kwa hii mateso yao: (Luka 21, 16 na 16-18; Waebrania 10, 36 na 12,1).

Msingi katika uzima wa Bwana Yesu Kristu ni sikitiko (uchungu) ya kama sisi ni watu wenye zambi. (Luka 18,13). Yeye hakukuwa na kazi ya ufarisayo, lakini kwa ajili ya sikitiko ya zambi yake alisamehewa kwa Bwana Yesu Kristu.

Tunawatakia na kuomba kwa Mwenyezi Mungu kusudi awangazie akili na roho zenu kwa kurudi katika kanisa ya kweli ya Bwana Yesu Kristu, kama munapenda wokovu wenu. Kwa sababu inje ya kanisa Orthodokse hakuna wokovu.

Kama kazi ya Bwana Yesu Kristu mu dunia ni ya kuokoa na kutakasa watu sisi tunauliza ma jamaa yote wa Protestanti watakatifu ngapi wenye kuwa na ma Kanisa yao? Miili yao yanabaki mzima bila kuoza sawa vile wanabaki watakatifu wa Orthodoksi? Wanafanya miujiza

mpaka sasa? Kama munapenda kufahamu na kujua Kanisa Orthodokse ile mwendo yenu itakuwa ya kwanza kwa kupata wokovu wenu.

**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU**
**HELLAS (GREKIA)**
**2000**